JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI (DSEE) 2020

## 721 KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI (DSEE) 2020

## 721 KISWAHILI

*Kimechapishwa na;*

Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624, Dar es Salaam,
Tanzania.

**©Baraza la Mitihani la Tanzania, 2020**

**Haki zote zimehifadhiwa**.

**YALIYOMO**

DIBAJI ..... iv
1.0 UTANGULIZI ..... 1
2.0 TATHMINI YA KILA SWALI ..... 2
2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi (Taaluma na Utaalamu) ..... 2
2.1.1 Swali la 1: Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili ..... 2
2.1.2 Swali la 2: Uhakiki wa Kazi za Fasihi ..... 5
2.1.3 Swali la 3: Zana za Kufundishia na Kujifunzia ..... 7
2.1.4 Swali la 4: Matamshi na Lafudhi ..... 10
2.1.5 Swali la 5: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia ..... 12
2.1.6 Swali la 6: Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili ..... 14
2.1.7 Swali la 7: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia ..... 17
2.1.8 Swali la 8: Maendeleo ya Kiswahili ..... 19
2.1.9 Swali la 9: Ufahamu ..... 22
2.1.10 Swali la 10: Upimaji ..... 25
2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha (Taaluma) ..... 27
2.2.1 Swali la 11: Fasihi ..... 27
2.2.2 Swali la 12: Maendeleo ya Kiswahili ..... 32
2.2.3 Swali la 13: Matamshi na Lafudhi ..... 36
2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha (Utaalamu) ..... 40
2.3.1 Swali la 14: Upimaji ..... 40
2.3.2 Swali la 15: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia ..... 45
2.3.3 Swali la 16: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Kiswahili ..... 50
3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU CHA WATAHINIWA KWA MADA ..... 55
4.0 HITIMISHO ..... 56
5.0 MAPENDEKEZO ..... 57
*Kiambatisho* ..... 58

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kutoa kitabu hiki kinachohusu taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa kuhitimu Stashahada ya Ualimu wa Sekondari katika somo la Kiswahili mwaka 2020. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho kwa walimu tarajali, wakufunzi, watunga sera, wakuza mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna watahiniwa walivyojibu maswali mbalimbali.

Taarifa hii ni tathmini ya mwisho inayoonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Kimsingi, majibu ya watahiniwa ni uthibitisho wa maarifa ambayo walipata au walishindwa kupata walipokuwa katika mafunzo ya Ualimu.

Uchambuzi utakaowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuchangia katika kuelewa zaidi sababu za watahiniwa kufanya vizuri, kwa kiwango cha wastani au hafifu. Taarifa hii inaonesha baadhi ya sababu zilizowafanya watahiniwa wengi kufanya vizuri, kama vile; kuelewa maelekezo na matakwa ya swali, kuwa na maarifa na ujuzi katika kujieleza kwa ufasaha na kuwa na uelewa wa mada mbalimbali zilizotahiniwa. Aidha, sababu zilizowafanya watahiniwa wachache kutokufanya vizuri zimefafanuliwa. Sababu hizo ni kama vile; kutokuelewa matakwa ya swali, kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada zilizotahiniwa, uwezo mdogo wa watahiniwa kujieleza kwa kutumia lugha fasaha na udhaifu katika kuelewa dhana zinazohusiana na somo la Kiswahili.

Taarifa hii itawawezesha viongozi wa elimu, viongozi wa vyuo, wakufunzi na walimu tarajali kupata mbinu stahiki zitakazosaidia kuboresha kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika mitihani ijayo.

Mwisho, Baraza linapenda kuwashukuru maafisa mitihani, wakufunzi wa somo na wengine wote waliohusika katika kutayarisha taarifa hii.

Dkt. Charles Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inalenga kuchambua viwango vya kufaulu vya watahiniwa katika mtihani wa somo la Kiswahili uliofanyika Julai, 2020. Mtihani huu ulikuwa na maswali 16 yaliyogawanywa katika sehemu A, B, na C ambapo sehemu A ilikuwa na maswali yaliyohusu mada za *Taaluma* na *Utaalamu wa Kufundisha Kiswahili kwa ngazi ya Sekondari*. Katika Sehemu B maswali yalihusu mada za *Taaluma ya Kufundisha Kiswahili* na yaliyohusu mada za *Utaalamu wa Kufundisha Kiswahili* yaliwekwa sehemu C.

Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) ambapo kila swali lilikuwa na alama 4. Mtahiniwa alipaswa kujibu maswali yote na jumla ya alama za sehemu hii ilikuwa ni 40. Sehemu B ilikuwa na maswali matatu (3) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili (2) na kila swali lilikuwa na alama 15 hivyo, kufanya jumla ya alama katika sehemu hii kuwa 30. Aidha, sehemu C ilikuwa na maswali matatu (3) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili (2) na kila swali lilikuwa na alama 15. Hivyo, jumla ya alama za sehemu hii zilikuwa 30. Kwa ujumla, mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali kumi na manne (14) kati ya kumi na sita (16).

Mtihani huu ulikuwa na viwango vitatu vya ufaulu ambapo kiwango kizuri kilianzia alama 70 hadi 100, kiwango cha wastani alama 40 hadi 69 na kiwango hafifu alama 0 hadi 39.

Watahiniwa waliosajiliwa kufanya mtihani wa Kiswahili kwa mwaka 2020 walikuwa 704. Kati yao, watahiniwa 697 sawa na asilimia 99.0 ya watahiniwa waliosajiliwa, walifanya mtihani. Aidha, watahiniwa 07 sawa na asilimia 1.0 hawakufanya mtihani. Watahiniwa waliofaulu kwa daraja A hadi D ni 692 sawa na asilimia 99.3 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Vilevile, watahiniwa 05 sawa na asilimia 0.7 walipata daraja F. Kiwango hiki cha ufaulu ni kizuri ikilinganishwa na mwaka 2019 ambapo asilimia 99.07 ya watahiniwa waliofanya mtihani huo, walifaulu kwa daraja A hadi D. Hivyo, ufaulu umeongezeka kwa asilimia 0.21 kwa mwaka 2020. Sehemu inayofuata ni tathmini ya kila swali ambapo viwango vya kufaulu vya watahiniwa vimebainishwa.

## 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI

Sehemu hii inahusu uchambuzi wa kina kwa kila swali na majibu yaliyotolewa na watahiniwa kwa kuonesha maswali yaliyofanywa vizuri, kwa wastani na vibaya. Aidha, sababu za ufaulu kwa kila kiwango yaani kizuri, wastani na hafifu kwa watahiniwa zimeelezwa bayana kwa kila swali. Vilevile, sampuli za majibu ya watahiniwa waliofanya vizuri au vibaya katika kila swali zimewasilishwa ili kuonesha majibu sahihi na yasiyo sahihi kwa kila swali.


Swali litaelezwa kwamba limejibiwa vizuri ikiwa theluthi mbili (2/3) na zaidi ya watahiniwa wamelijibu vizuri na kupata alama 3-4 na litaelezwa kuwa limejibiwa vibaya ikiwa theluthi mbili (2/3) na zaidi ya watahiniwa ndio waliopata alama 0-1.5 . Aidha, swali litaelezwa kuwa limejibiwa kwa kiwango cha wastani ikiwa idadi ya watahiniwa waliopata alama 2-2.5 inazidi theluthi moja (1/3) na haikuzidi theluthi mbili (2/3).

## 2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi (Taaluma na Utaalamu)

Sehemu hii ilikuwa na maswali kumi (10) yaliyohitaji majibu mafupi ambayo yalitungwa kutoka katika mada za *Taaluma* na *Utaalamu wa Kufundisha Kiswahili*. Mtahiniwa alipaswa kujibu maswali yote. Kila swali lilikuwa na uzito wa alama nne (4) hivyo, kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama arobaini (40).

### 2.1.1 Swali la 1: Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutaja mambo manne ya kuzingatia wakati wa kuandaa muhtasari wa somo la Kiswahili.Watahiniwa wote (100%) waliofanya mtihani walijibu swali hili. Aidha, swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango cha wastani kwani asilimia` 47.0 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4. Ufaulu wa watahiniwa hao ni kama inavyoonekana katika Chati Na.1.




**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1.*

Watahiniwa 370 sawa na asilimia 53.0 walipata alama 0 hadi 1.5 kutokana na kutokuelewa matakwa ya swali. Baadhi yao, walichanganya maudhui inayopatikana katika muhtasari wa somo la Kiswahili na mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa muhtasari huo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja kama vile; *ujuzi, malengo mahsusi, vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji na shughuli za upimaji* badala ya kutaja mambo manne ya kuzingatia wakati wa kuandaa muhtasari wa somo la Kiswahili ambayo ni; *mada zinazoandaliwa zizingatie kiwango cha uelewa wa wanafunzi, uzingatie malengo ya elimu ya taifa, uzingatie masuala mtambuka, uzingatie mazingira ya mwanafunzi anayekusudiwa kujifunza somo la Kiswahili na muda unaotumika kufundisha mada mbalimbali katika kiwango husika* na hivyo, kusababisha kupata alama 0.


Aidha, watahiniwa wengine hawakuwa na uelewa juu ya mada ya Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili hususan katika kipengele cha *muhtasari* kwani waliandika majibu ya kubuni ambayo ni kinyume kabisa na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika; *lengo mahsusi, lengo kuu, ujuzi na ufahamu* ,mwingine aliandika; *mtaala, vifaa vya kufundishia na kujifunzia kama chaki, ubao na kalamu, wataalamu tofauti wa elimu na taasisi mbalimbali za elimu* na mwingine aliandika; *somo husika, lugha iliyotumika na umahili*. Vilevile, wengine walifanikiwa kutaja hoja moja sahihi kati ya nne na kupata alama 1. Kielelezo Na.1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.


1 Mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa Muhtasari wa somo la kiswahili ni
i/ Kuwepo kwa Kitabu cha kiada na ziada.
ii/ Kuwepo kwa kalenda ya shule na serikali.
iii/ Kuwepo na muhtasari wa somo.
iv/ Kuwe na vitabu vya rejea.

**Kielelezo Na. 1.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 1.

Kielelezo Na. 1.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyetaja vifaa vinne vya mtaala wa somo la Kiswahili badala ya mambo manne ya kuzingatia wakati wa kuandaa muhtasari wa somo la Kiswahili.

Vile vile, watahiniwa wachache sawa na asilimia 25.3 walijibu vizuri swali hili na kupata alama 3 hadi 4. Watahiniwa hao, waliweza kutaja mambo matatu hadi manne ya kuzingatia wakati wa kuandaa muhtasari wa somo la Kiswahili. Hii inathibitisha kuwa, watahiniwa hawa walielewa vizuri dhana ya muhtasari pamoja na matakwa ya swali. Mambo yaliyotajwa na watahiniwa hao ni pamoja na; *uzingatie maswala mtambuka, uzingatie muda utakaotumika kufundisha mada mbalimbali katika kiwango husika na uwepo wa majedwali yanayoonyesha njia, mbinu na rejea*. Kielelezo Na.1.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


1. Mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa muhtasari wa somo la Kiswahili.
(i) Malengo ya kufundisha somo la Kiswahili.
(ii) Kiwango cha elimu ambayo muhtasari unaandaliwa
(iii) Jamii au mazingira husika ya jamii ambayo muhtasari unalenga kutumika.
(iv) Falsafa ya elimu kwa wakati husika.


**Kielelezo Na.1.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 1.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 21.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 2 hadi 2.5 kutokana na kutokuandika majibu yanayojitosheleza. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walitaja mambo mawili sahihi badala ya manne kama swali lilivyotaka na wengine walitaja mambo mawili sahihi na mengine hayakuwa sahihi.

Vilevile, wengine walichanganya mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa muhtasari wa somo la Kiswahili na umuhimu wa mwalimu kutumia muhtasari wa somo la Kiswahili hivyo, kupata alama za wastani.

### 2.1.2 Swali la 2: Uhakiki wa Kazi za Fasihi

Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua maana ya tamathali za semi zifuatazo na kutoa mfano kwa kila moja: (a) Mubaalagha (b) Sitiari (c) Tashbiha na (d) Tashtiti.Watahiniwa wote (697) waliofanya mtihani, walijibu swali hili. Asilimia 37.3 walipata alama 2 hadi 4 na kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango hafifu kama inavyoonekana katika Chati Na.2.





**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2.*

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, watahiniwa 437 sawa na asilimia 62.7 walipata alama 0 hadi 1.5. Baadhi yao, hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu kipengele cha tamathali za semi katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa maelezo ya tamathali za semi tofauti na zilizoulizwa kwenye swali husika. Mtahiniwa huyo, alitoa maana ya Mubaalagha kuwa *ni kitendo cha kuficha jambo fulani* badala ya *uwekaji wa chuku katika kisa ili kuonesha msisitizo wa kitu kinachosemwa*. Maana iliyotolewa inafafanua tamathali ya semi iitwayo *tafsida*. Vile vile, alieleza kuwa *sitiari ni kitendo cha kulinganisha vitu viwili tofauti kwa mfano mithili ya.....* badala ya *kulinganisha vitu viwili bila kutumia viunganishi*. Maana iliyotolewa inafafanua tamathali ya semi iitwayo tashbiha ingawa haikuwa sahihi.

Aidha, alieleza maana ya tashbiha kuwa *ni kitendo cha kuipa kitu sifa ya kutenda jambo kama binadamu kwa mfano moyo ulitiririka machozi* badala ya *tamathali ya semi*

*ambayo hulinganisha vitu kwa kutumia viunganishi "kama vile" na "mithili ya"*. Maelezo hayo yanatoa maana ya tamathali ya semi iitwayo *tashsisi*. Pia, alieleza kuwa tashtiti *ni kitendo cha kulinganisha vitu viwili bila kutumia viunganishi* badala ya *kitendo cha kuuliza swali ilihali jibu linajulikana na muuliza swali* ambapo maana iliyotolewa ni ya tamathali ya semi inayoitwa *tashbiha*. Kwa ujumla, mtahiniwa huyo alitoa maana ya tafsida badala ya mubaalagha, tashbiha badala ya sitiari, tashihisi badala ya tashbiha na tashbiha badala ya tashtiti.

Halikadhalika, wapo watahiniwa wachache ambao walitoa majibu ambayo hayahusiani na dhana ya tamathali za semi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua maana ya mubaalagha kuwa *ni maneno yenye msisitizo na sitiari ni maneno yanayofuatana kwenye mlolongo wa vitu*. Wengine walifanikiwa kutoa maana na mfano sahihi katika kipengele kimoja tu na kupata alama 1. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi kutokana na uelewa mdogo wa mada iliyotahiniwa.


2. (a) Mubaalagha, ni tamathali za memi ambazo hutumika ku kejeri

(b) Sitiari, Ni kutumia neno bila kiunganishi.

(c) Tashbiha, Kutumia neno na kiunganishi mfano mzuri kama .


**Kielelezo Na. 2.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika Swali la 2.

Katika kielelezo Na. 2.1, mtahiniwa alishindwa kufafanua tamathali ya semi katika kipengele (d) Tashtiti. Aidha, maana alizotoa katika vipengele vingine hazikuwa sahihi na alishindwa kuweka mfano kama yalivyokuwa matakwa ya swali.

Aidha, asilimia 22.7 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu walipata alama 2 hadi 2.5. Miongoni mwao, walifafanua maana ya tamathali za semi katika vipengele viwili na kutoa mifano kwa usahihi na kushindwa vingine na wengine walitoa maana za tamathali za semi bila kutoa mifano hivyo, kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, asilimia 14.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 3 hadi 4 kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya *tamathali za Semi*. Vile vile, walielewa vizuri matakwa ya swali hivyo, waliweza kufafanua maana ya tamathali za semi katika vipengele vitatu hadi vinne huku wakitoa mifano kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu kama ifuatavyo; (a) *mubaalagha ni uwekaji wa chuku katika kisa ili kuonesha msisitizo wa kitu kinachosemwa mfano; walikufa kama*

*inzi*, (b) *Sitiari ni tamathali inayolinganisha kitu kimoja na kingine kwa kuvifanya viwe sawasawa bila kutumia viunganishi mfano; Salama ni malaika ameumbika haswa*, (c) *Tashbiha ni tamathali inayolinganisha kitu kimoja na kingine. Ulinganishi huu unafanywa kwa kutumia viunganishi kama vile kama*, mfano Asha ni mweusi kama mkaa na (d) *Tashtiti ni mbinu ya kisanaa ambayo mhusika huuliza swali ambalo jibu lake analifahamu* mfano: *hivi ni kweli Corona ni hatari?*. Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa mwingine aliyefafanua maana za tamathali za semi na kutoa mifano kwa usahihi.


2. (a) Mubahlagha ni kitendo ni kitendo cha kutia chukui au chumvi katika kazi ya fasihi. Mfano: Walihudhuria maelfu ya watu katika harusi yake.

(b) Sitiari ni ~~ku~~ tamathali ya semi ambayo hulinganisha vitu bila kutumia viunganisha ~~kam~~ mfano Kama, mithili ya, kama vile. Mfano: Juma ni simba


(c) Tashbiha ni tamathali ya semi ambayo hulinganisha vitu kwa kutumia viunganishi kama vile, mithili ya: Mfano, Alinuka mithili ya simba amnukae pofu.

(d) Tashtiti- Ni tamathali ya semi ambayo huuliza maswali yasiyohitaji majibu. Mfano, Hivi Magufuli ndio Rais wetu?

**Kielelezo Na.2.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 2.


### 2.1.3 Swali la 3: Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kutaja athari nne zinazoweza kutokea iwapo mwalimu atatumia zana halisi bila tahadhari katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji. Asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 2 hadi 4 kwa asilimia 90.9 hivyo, kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Chati Na. 3 inafafanua viwango vya ufaulu vya watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 551 sawa na asilimia 79.0 walipata alama 3 hadi 4. Watahiniwa hao, waliweza kukidhi matakwa ya swali kutokana na uelewa mkubwa waliokuwa nao juu ya mada ndogo ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili*. Waliweza kutaja athari tatu hadi nne zinazoweza kutokea iwapo mwalimu atatumia zana halisi bila tahadhari katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja hoja kama vile; *kusababisha ajali, wasiwasi kwa wanafunzi, nidhamu ya darasa kushuka* na *wanafunzi kuanza kupiga kelele na hata kutoka nje ya darasa*. Kielelezo Na. 3.1. ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri kulingana na matakwa ya swali.





**Kielelezo Na. 3.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 3.

Vilevile, watahiniwa 82 sawa na asilimia 11.8 walipata alama 2 hadi 2.5. Watahiniwa wengi wa kundi hili, walitoa hoja mbili sahihi na hoja nyingine zisizo sahihi. Pia, wengine walichanganya athari za mwalimu kutokutumia zana na athari zinazoweza

kutokea iwapo mwalimu atatumia zana halisi bila tahadhari katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji na kusababisha kupata alama za wastani. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alitaja hoja kama vile; *wanafunzi kushindwa kutunza kumbukumbu ya kudumu, wanafunzi kutokuwa wabunifu, kuchukia somo na wanafunzi kuwa na wasiwasi.*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 64 sawa na asilimia 9.2% walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Baadhi yao, walishindwa kujibu kulingana na matakwa ya swali kwa sababu wapo walioandika faida za kutumia zana darasani kama vile; *wanafunzi kupata kumbukumbu ya kudumu, kuwa wadadisi, kufikiwa malengo mahsusi na kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji* badala ya kutaja athari nne za kutumia zana halisi bila tahadhari ambazo ni; zana *inaweza kupoteza usikivu wakati wa matumizi pale mwalimu atakapotumia wanyama kama mbwa, inaweza kusababisha ajali endapo mwalimu atatumia vifaa kama mkasi au visu , inaweza kutumia muda mrefu pale itakapolazimika kusafiri kwa umbali mrefu* na *inaweza kusababisha matabaka baina ya wanafunzi iwapo mwanafunzi atashindwa kuchangia kununua au kusafirisha*.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, majibu mengine yaliyotolewa na baadhi ya watahiniwa yalitokana na uelewa mdogo wa mada ndogo ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili* hivyo, kuwafanya kutoa majibu yasiyohusiana kabisa na athari za mwalimu kutumia zana halisi bila tahadhari. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja hoja kama vile; *wanafunzi kuondoka na zana, wanafunzi kuchezea zana* na *kuwa makini kuangalia zana*. Mtahiniwa mwingine aliandika hoja nyingine ambazo ni; *mwalimu atashindwa kujiamini, kufuata hatua za ufundishaji na ujifunzaji kupitia zana hiyo, hatakuwa na ujuzi na atatumia muda mwingi katika kuitumia*. Aidha, watahiniwa wengine walifanikiwa kutaja athari moja sahihi na kushindwa nyingine hivyo kupata alama hafifu. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



3: i) kutokujiamini.
ii) Kutoelewaka kwa zana
iii) kufundisha njo ya mada
iv) Kutofuata mririko sahihi

**Kielelezo Na. 3.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 3.

Katika kielelezo Na. 3.2, mtahiniwa alitaja athari zitakazojitokeza iwapo mwalimu ataandaa zana isiyo bora badala ya athari zinazoweza kutokea iwapo mwalimu atatumia zana halisi bila tahadhari katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji.

### 2.1.4 Swali la 4: Matamshi na Lafudhi

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa kifupi maana ya dhana zifuatazo: (a) Kiimbo na (b) Mkazo.Watahiniwa wote (100) waliofanya mtihani walijibu swali hili. Miongoni mwao, asilimia 61.8 walipata alama 2 hadi 4 hivyo, kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango cha wastani kama inavyoonekana kwenye chati Na.4.





**Chati Na. 4:** *Ufaulu kwa Watahiniwa katika Swali la 4.*

Watahiniwa 266 Sawa na asilimia 38.2 ya watahiniwa wote waliojibu swali hili walipata alama 0 hadi 1.5. Baadhi ya watahiniwa hao, hawakuweza kutimiza matakwa ya swali kwani walitoa maelezo yasiyohusiana na istilahi zilizoulizwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichanganya dhana ya ushairi na matamshi kwani aliandika kuwa*; kiimbo ni ubeti wa mwisho kwenye shairi ambao huimbika na mkazo ni mstari unaojirudiarudia katika shairi* badala ya kueleza kuwa ni*; utaratibu maalumu wa kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti wakati wa kuzungumza. Kwa kawaida, kiimbo hubeba maana fulani ya kile ambacho kinazungumzwa* badala ya *kiwango cha nguvu inayotumika katika utamkaji wa silabi. Silabi yenye mkazo kuwa inatamkwa kwa nguvu nyingi zaidi kuliko ile isiyokuwa na mkazo.* Mwingine aliandika kuwa; *kiimbo ni kiambishi tamati katika kimalizikio cha ubeti wa ushairi au kurudiarudia beti katika ushari* na *mkazo ni sauti zinazotamkwa kwa kutumia nguvu katika mstari wa mwisho wa ubeti wa shairi*.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa wengine hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana mbalimbali katika mada ya *Matamshi na Lafudhi* hivyo, walitoa maana dhaifu ya dhana walizoulizwa na kusababisha kupata alama hafifu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza maana ya *kiimbo kuwa ni kupanda*

*na kushuka kwa mawimbi* ambapo alishindwa kumalizia ni mawimbi ya nini*? na mkazo ni hali ya kutamka maneno kwa nguvu*. Pia, watahiniwa wengine waliandika majibu ambayo hayahusiani kabisa na dhana ya *Matamshi na Lafudhi*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kuwa; *kiimbo ni maneno yanayooneshwa mwisho wa kitabu yanayokolezwa wino mweusi* na *mkazo ni kutumia nguvu ya ziada kusisitiza jambo fulani* na mwingine aliandika kuwa; *kiimbo ni ujazo wa sauti zinazotumika katika uimbaji au zinazotumiwa na mtumiajai wa lugha na mkazo ni msisitizo wa jambo fulani katika uimbaji*. Kielelezo Na.4.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali.



4. (a) Kiimbo.
Haya ni maneno yanayoandikwa kwenye kamusi kutoa maana ya neno.
Mf:
Ua: ni kitendo cha kutoa uhai wa mtu.
(b) Maneno yanayoandikwa kwa kutoa msisitizo juu ya kitu au jambo fulani katika kamusi.

**Kielelezo Na 4.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 4.

Kielelezo Na.4.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyeeleza kwa kifupi maana ya kiimbo na mkazo kwa kuhusianisha na dhana ya kamusi badala ya Matamshi na Lafudhi.

Vile vile, watahiniwa 221 sawa na asilimia 31.7 walipata alama 2 hadi 2.5 kwa kuwa miongoni mwao, walielezea kipengele kimoja kwa usahihi na kuacha kingine na wengine walishindwa kueleza maana zinazojitosheleza. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuwa kiimbo ni *hali ya kupanda na kushuka kwa sauti* na mkazo *ni hali ya kutamka maneno kwa kuweka msisitizo*.

Hata hivyo, asilimia 30.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 3 hadi 4. Watahiniwa wa kundi hili, walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya dhana mbalimbali katika mada ya *Matamshi na Lafudhi*. Walielezea kwa kifupi maana ya dhana ya kiimbo na mkazo kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuwa *kiimbo ni utaratibu maalumu wa kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti wakati wa kuzungumza. Kwa kawaida, kiimbo hubeba maana fulani ya kile ambacho kinazungumzwa*. Aidha, alielezea dhana ya *mkazo* kuwa ni; *kiwango cha nguvu inayotumika katika utamkaji wa silabi. Silabi yenye mkazo huwa inatamkwa kwa nguvu nyingi zaidi kuliko ile isiyokuwa na mkazo*. Kielelezo Na.4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa mwingine aliyejibu vizuri swali hili.



4. a/ Kiimbo ; ni kiwango cha kupanda na kushuka kwa sauti wakati wa kutamka maneno. kuna kiimbo cha amri, kiimbo cha maelezo, kiimbo cha kuuliza na kiimbo cha mshangao.
mfano: Njoo upesi!!


b/ Mkazo ; ni nguvu ya ziada inayotiwa katika neno wakati wa kutamka maneno. Mfano Mwanafunzi, Cheza

**Kielelezo Na.4.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 4.

Kielelezo Na.4.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyeelezea dhana ya kiimbo na mkazo kwa usahihi. Aidha, katika maana iliyotolewa, mtahiniwa alieleza kuwa; mkazo ni nguvu inayotiwa katika neno badala ya silabi wakati wa kutamka maneno badala ya neno. Pamoja na dosari hiyo, mtahiniwa ameonekana kuwa na uelewa kuwa kukaza ni kitendo cha kuongeza nguvu wakati wa utamkaji.

### 2.1.5 Swali la 5: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia


Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kuchambua mbinu nne zinazoweza kutumika sambamba na mhadhara wakati wa tendo la ufundishaji na ujifunzaji. Swali lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani. Watahiniwa waliopata alama 2 hadi 4 ni asilimia 69.9 hivyo, kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Chati Na. 5 inafafanua viwango vya ufaulu.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5.*

Baadhi ya watahiniwa ambao ni sawa na asilimia 35.0 walipata alama 2 hadi 2.5 kutokana na sababu mbalimbali. Sababu hizo ni pamoja na kushindwa kutoa maelezo ya kina, kutoa hoja mbili sahihi na nyingine zisizo sahihi na kutaja mbinu nne zinazoweza kutumika sambamba na mhadhara badala ya kuchambua mbinu hizo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja mbinu kama vile; *majadiliano, mwaliko wa mgeni, onesho mbinu na maswali na majibu* bila kutoa maelezo. Pia, wengine waliweza kuchambua hoja mbili sahihi badala ya nne hivyo kupata alama za wastani.

Vile vile, watahiniwa 240 sawa na asilimia 34.9 walijibu swali hili vizuri na kupata alama 3 hadi 4 kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mbinu mbalimbali za kufundishia na kujifunzia Kiswahili. Hivyo, waliweza kuchambua mbinu tatu hadi nne zinazoweza kutumika sambamba na mhadhara wakati wa tendo la ufundishaji na ujifunzaji kama vile; *mbinu ya kualika mgeni*. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.


(i) Maswali na majibu, hii ni mbinu ambayo inamshirikisha mwanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji. Mbinu hii inaweza kutumika sambamba na mbinu ya mhadhara pale ambapo baada ya mhadhara mwalimu anaruhusu maswali na kisha kuyajibu

(ii) Majadiliano ya pamoja. Hii ni mbinu inayoweza kutumika sambamba na mbinu ya mhadhara pale ambapo mwalimu anaweza kuruhusu kujadili mada kwa pamoja


(iii) Bungua bongo, hii ni mbinu ambayo hutumiwa na mwalimu kwa kuuliza maswali yanayohitaji majibu mafupi ya papo kwa papo ili kupata maarifa ya awali waliyonayo wanafunzi kabla ya kuanza mbinu ya mhadhara wakati wa ufundishaji na ujifunzaji

(iv) Onesho mbinu, hii ni mbinu ambayo hutumiwa na mwalimu kwa kushirikiana na wanafunzi kuonesha namna ya kufanya jambo mbinu hii inaweza kwenda sambamba na mbinu ya mhadhara, kwa kuonesha namna ya kufanya jambo.

**Kielelezo Na. 5.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 5.

Hata hivyo, watahiniwa 212 sawa na asilimia 30.1 walijibu swali hili na kupata alama 0.5 hadi 1.5. Miongoni mwao, hawakuelewa matakwa ya swali hivyo, walishindwa kueleza mbinu nne zinazoweza kutumika sambamba na mhadhara wakati wa tendo la ufundishaji na ujifunzaji. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika mbinu ambazo haziwezi kutumika sambamba na mhadhara kama vile; *ziara, changanya kete na matembezi ya galari* ingawa ni mbinu zinazotumika katika ufundishaji na ujifunzaji.

Aidha, watahiniwa wengine hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mbinu mbalimbali za kufundishia na kujifunzia Kiswahili kwani walitoa majibu yasiyoendana kabisa na swali. Mfano, mtahiniwa mmoja alitaja mbinu moja inayoweza kutumika sambamba na mhadhara kisha kuchambua aina za utungaji wa maandishi katika hoja tatu kitu ambacho ni kinyume cha matakwa ya swali na hivyo, kupata alama 0.5. Majibu ya mtahiniwa huyo yalikuwa; *Kualika mgeni, Risala, Hotuba* na *Insha*. Kielelezo Na. 5.2 ni mfano wa majibu yasiyo sahihi yaliyotolewa na mmoja wa watahiniwa.



5. Mbinu zinazoweza kutumika wakati wa mhadhara
i) Kusikiliza kwa umakini.
ii) Kuandika mambo ya muhimu.
iii) Kumtazama mzungumzaji ili kuona baadhi ya vitendo anavyo vitumia.
iv) Kuuliza maswali pasipo kuchoka.

**Kielelezo Na. 5.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 5.

Kielelezo Na. 5.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyetaja mbinu nne atakazotumia mwanafunzi kuelewa somo iwapo mwalimu atafundisha kwa kutumia mbinu ya mhadhara badala ya kuchambua mbinu nne zinazoweza kutumika sambamba na mhadhara wakati wa tendo la ufundishaji na ujifunzaji.


### 2.1.6 Swali la 6: Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili

Swali hili lilimtaka mtahiniwa aeleze mambo mawili yanayosababisha utata katika sentensi. Asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili ambapo asilimia 94.7 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4 na kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya ufaulu kwa asilimia.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu kwa Watahiniwa katika Swali la 6.*

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, watahiniwa 524 sawa na asilimia 75.2 walijibu swali hili vizuri na kupata alama 3 hadi 4 kwa sababu waliweza kuelezea kwa usahihi mambo mawili yanayosababisha utata katika sentensi na kutoa mfano kwa kila moja. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea mambo hayo kuwa ni; *kudondosha au kuongeza vipashio katika neno* na *kutokuzingatia taratibu za uandishi*. Wengine waliandika sababu nyingine ambayo ni; *matumizi ya kiambishi cha utendeshi (-i-/-e-) kwa mfano bibi amempikia mjukuu wake vitumbua*. Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.


6. i) Neno kuwa na maana zaidi ya moja, endapo neno moja litakuwa na maana zaidi ya moja basi sentensi yaweza kuwa tata
Kwa mfano.
Mtoto ameleta kaa.
Katika sentensi hiyo neno kaa laweza kuwa na maana ya kipande cha kuni cha moto na maana nyingine kuwa ni mdudu aitwaye kaa.
ii) Matumizi ya lugha ya picha.
Lugha ya picha katika sentensi huweza kusababisha utata kwa sababu lugha hiyo ya picha huficha maana ya neno halisi iliyo kusudiwa.
Mfano: Nyumbani kwangu kuna ua zuri.
Neno ua linaweza kuwa na maana ya mmea uliopandwa nyumbani;
Au kutoa maana ya kuwa na binti mrembo nyumbani


**Kielelezo Na. 6.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 6.

Katika kielelezo Na. 6.1, mtahiniwa alieleza neno kuwa na maana zaidi ya moja na matumizi ya lugha ya picha kama mambo yanayosababisha utata katika sentensi. Aidha, alitoa mfano sahihi kwa kila hoja.

Vilevile, asilimia 19.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu walipata alama 2 hadi 2.5. Miongoni mwao, walielezea hoja moja na kutoa mfano, wengine walishindwa kutoa maelezo yanayojitosheleza kwa hoja zote mbili na wengine walifanikiwa kuelezea hoja zote mbili na kushindwa kuweka mfano kama yalivyokuwa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza hoja kama vile; *neno kuwa na maana zaidi ya moja katika sentensi husababisha utata* na *iwapo taratibu za uandishi hazitafuatwa utata hutokea pia.*

Hata hivyo, watahiniwa wachache (5.3%) walipata alama 0 hadi 1.5. Baadhi yao, hawakuelewa matakwa ya swali kwani walichanganya mambo yanayosababisha utata katika sentensi na mambo yanayosababisha makosa ya kisarufi katika mawasiliano. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza hoja kama vile; *athari za lugha mama na kutokufuata mpangilio wa maneno katika sentensi mfano, mpole mtoto anacheza* badala ya kuelezea mambo mawili yanayosababisha utata ambayo ni; *kutokuzingatia taratibu za uandishi kama vile kutokuweka kituo au mkato mahali panapostahili* kwa mfano; *Baba Juma anakuja*, *kudondosha au kuongeza vipashio katika neno, matumizi ya lugha ya picha na matumizi ya kiambishi cha utendeshi (-i-/-e-) kwa mfano; Juma alimpigia John mpira*.

Aidha, watahiniwa wengine hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ndogo ya *Utata katika Mawasiliano* hivyo, walitoa hoja dhaifu na kupata alama hafifu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kueleza mambo yanayosababisha utata katika sentensi badala yake alitaja tu mfano wa maneno yanayosababisha utata na kutaja utata katika sentensi kama hoja. Mtahiniwa huyo aliandika kuwa; *utata wa neno kwa mfano sawasawa na utata wa sentensi.* Kielelezo Na. 6.2 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa yasiyo sahihi katika swali hili.



6(i) Rejesta mfano rejesta za mitihani mfn chochea
(ii) Misimu mfn misimu ya vijeo mf udaku

**Kielelezo Na. 6.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 6

Kielelezo Na. 6.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyetaja aina za rejesta na misimu badala ya kuelezea mambo yanayosababisha utata katika sentensi. Aidha, ametaja rejesta za mitaani mfano chochea na misimu ya njeo dhana ambazo sio sahihi.

### 2.1.7 Swali la 7: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia

Katika swali hili, mtahiniwa alipaswa kubainisha mbinu nne atakazotumia mwalimu kufanya tathmini ya somo darasani. Swali lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya kwani asilimia 28.4 pekee ya watahiniwa waliojibu swali hili ndio waliopata alama 2 hadi 4. Chati Na. 7 inafafanua viwango vya ufaulu vya watahiniwa.





**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 7.*

Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 492 sawa na asilimia 70.6 walipata alama 0 hadi 1.5 kwa sababu wengi wao, walichanganya mbinu atakazotumia mwalimu kufanya tathmini ya somo darasani na zana zinazotumika kufanya tathmini ya somo darasani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alibainisha *mkoba wa kazi, mazoezi ya darasani, mitihani na kazi mradi* badala ya kutaja mbinu atakazotumia mwalimu kufanya tathmini ya somo darasani ambazo ni; *vitendo vya upimaji atakavyofanya mwalimu darasani kama kushirikisha wanafunzi kwa kuuliza maswali, kutumia malengo mahsusi ya somo, tafakuri ya somo, mwitikio chanya wa wananfunzi* na *kuwaelekeza wanafunzi kutoa maoni kuhusiana na somo husika*. Majibu ya mtahiniwa huyo yanawakilishwa na mbinu moja tu ya vitendo vya upimaji atakavyofanya mwalimu darasani na hivyo kusababisha kupata alama 1. Majibu ya watahiniwa hao yanathibitisha kuwa, hawakuwa na uelewa

wa kutosha juu ya mbinu mbalimbali zinazoweza kutumika kufanya tathmini ya somo darasani.

Aidha, watahiniwa wengine waliandika majibu yasiyohusiana kabisa na mbinu za kufanya tathmini ya somo darasani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja kama vile; *utulivu na usikivu, haiba ya mwalimu, ukaaji wa mwalimu katika kufundisha* na *ukaaji wa wanafunzi darasani*. Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi kutokana na kutokuelewa matakwa ya swali.



7. i/ Kuuliza maswali.
ii/ Kuandaa kazi za makundi.
iii/ Kuwapa ka za nyumbani
iv/ Kufanya mtihani

**Kielelezo 7.1:** Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 7.

Katika kielelezo Na.7.1, mtahiniwa alibainisha njia nne atakazotumia mwalimu kufanya tathmini ya somo darasani badala ya mbinu nne atakazotumia mwalimu kufanya tathmini ya somo darasani. Aidha, njia hizo zinawakilishwa na mbinu moja ambayo ni vitendo vya upimaji atakavyofanya mwalimu darasani hivyo, akapata alama 1.

Vile vile, watahiniwa 115 sawa na asilimia 16.5 walipata alama 2 hadi 2.5 kwa kuwa walibainisha hoja za kubuni ambapo baadhi zilikuwa sahihi lakini nyingine hazikuwa sahihi. Aidha, wengine walitaja mbinu mbili za kufanya tathmini ya somo darasani kwa usahihi huku wakichanganya na mbinu za kufundishia na kujifunzia. Kwa mfano, majibu ya mtahiniwa mmojawapo yalikuwa; *mwalimu kufanya shughuli mbalimbali za upimaji kama mazoezi na maswali na majibu, kutumia malengo mahsusi ya somo, kufanya ziara na kualika mtaalam* na hivyo kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 90 sawa na asilimia 12.9 walipata alama 3 hadi 4. Watahiniwa hao, walijibu kulingana na matakwa ya swali kutokana na uelewa mkubwa waliokuwa nao juu ya mbinu mbalimbali zinazotumika kufanya tathmini ya somo darasani. Mathalani, mtahiniwa mmoja aliandika mbinu hizo kuwa ni; *kutumia malengo mahususi ya somo , tafakuri ya somo, mwalimu kutoa mazoezi mbalimbali* na *kupata mrejesho kutoka kwa wanafunzi mbalimbali*. Kielelezo Na.7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi.



7. (i) kuwauliza maswali wanafunzi kuhusiana na somo husika.
(ii) kutoa zoezi fupi baada ya kufundisha somo husika.
(iii) kumsimamisha mwanafunzi mmoja baada ya mwingine aeleze kwa ufupi alichojifunza ndani ya kipindi cha somo hilo.
(iv) kuangalia muitikio na uhirikiano unaotolewa na wanafunzi darasani wakati kufundisha na kujifunza somo la kiswahili'


**Kielelezo Na. 7.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 8

.

Katika Kielelezo Na. 7.2 mtahiniwa aliweza kubainisha mbinu nne atakazotumia mwalimu kufanya tathmini ya somo darasani ingawa mbinu mbili za mwanzo zinawakilishwa na mbinu ya *vitendo vya upimaji atakavyofanya mwalimu darasani*. Hivyo, kufanya majibu sahihi ya mtahiniwa huyo kuwa hoja tatu badala ya nne.

### 2.1.8 Swali la 8: Maendeleo ya Kiswahili

Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kufafanua kwa ufupi mitazamo ifuatayo kuhusu chimbuko la Lugha ya Kiswahili: (a) Chimbuko la Kiswahili ni Kameruni na (b) Chimbuko la Kiswahili ni Kongo. Swali lilijibiwa na watahiniwa wote (100%) waliofanya mtihani huu na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango cha wastani kwani asilimia 68.9 walipata alama 2 hadi 4. Chati Na. 8 inafafanua viwango vya ufaulu vya watahiniwa.





**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 8.*

Asilimia 35.0 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama 2 hadi 2.5. Watahiniwa hao, walishindwa kufafanua hoja kwa ufasaha na wengine kufafanua mtazamo katika kipengele kimoja na kuacha kingine hivyo kupata alama za wastani.

Vile vile, watahiniwa 217 sawa na asilimia 33.9 walipata alama 0 hadi 1.5. Miongoni mwao, hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* hususan katika kipengele cha Chimbuko la Lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea nadharia za *ushahidi wa Ally Idris, Ushahidi wa Fumo Lyongo, ushahidi wa Mark Guthrie na ushahidi wa vita ya watu weusi wa kaskazini* badala ya kueleza Chimbuko la Kiswahili ni Kameruni. Nadharia hiyo inaeleza kuwa; *Kameruni ni nchi iliyopo magharibi mwa Bara la Afrika ambapo karne nyingi zilizopita waliishi wabantu waliojishughulisha na biashara, ufugaji na kilimo. Lilitokea baa la njaa na kuwalazimu wabantu kusambaa wakitafuta malisho na kilimo hivyo wakajikuta wameingia Kongo na baadae walivuka mipaka na kuingia Afrika ya Mashariki. Inasemekana kwamba wabantu hao waliwasiliana kwa kutumia lugha ya Kiswahili*.

Aidha, nadharia ya chimbuko la Kiswahili ni Kongo inafafanua kuwa; *kwa sababu miaka ya zamani kulikuweko na waswahili walioishi Kongo kutokana na vita na njaa huko Kongo wabantu hao walisambaa kote Afrika Mashariki na lugha iliyokuwa ikitumika inasemekana kuwa ilikuwa lugha ya Kiswahili.* Mtahiniwa mwingine alifafanua kimakosa chimbuko la Kiswahili kuwa ni Kameruni *kwa sababu lugha ya kikameruni inaendana na Kiswahili na chimbuko la Kiswahili ni Kongo kwa sababu wakongo walipenda sana Kiswahili*. Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.



8. Chimbuko ya la Kiswahili; Miaka ni lugha ya Kiswahili kilipo anzia- hivyo basi lugha ya Kiswahili chimbuko lako ni Ujerumani. Kuna tena niujerumani na Kongo kwa sababu zifuatazo kuanza na Ujerumani na kumalizia na Kongo, nazo ni :-

Msamiati; katika ushahidi wa kihistoria kuna kuelezwa kwa kuna baadhi ya msamiati ya lugha ya kiswahili inafanana na lugha ya kijerumani hivyo ndipo walipo dai kwa kiswahili chimbuko lako ni Ujerumani -

Muundo; pia hata muundo wa lugha ya Kiswahili unafanana sana na lugha ya kijerumani hivyo wanahistoria walidai kua lugha ya Kiswahili chimbuko lako ni Ujerumani. hivyo basi kwa kumalizia na chimbuko la kiswahili ni Kongo. kwa sababu zifuatazo'

Ki msamiati; Hivyo msamiati wa lugha ya kiswahili una fanana na lugha ya Kongo hivyo ndipo walipo sema kwa lugha ya kiswahili asili chimbuko lako ni Kongo pia hata hivyo kizazi cha kikosa mashiko baada ya kukosa ushahidi wa kitayansi -

**Kielelezo Na. 8.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 8.


Kielelezo Na. 8.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyefafanua chimbuko la Kiswahili kuwa ni Kijerumani katika misingi ya kimsamiati na kimuundo badala ya kufafanua mtazamo wa (a) Chimbuko la Kiswahili ni Kameruni na (b) Chimbuko la Kiswahili ni Kongo jambo linaloonesha kuwa hakuelewa matakwa ya swali.

Hata hivyo, asilimia 33.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 3 hadi 4. Watahiniwa hao, waliweza kufafanua kwa ufasaha mitazamo ya chimbuko la Kiswahili kuwa ni Kameruni na Kongo. Hii inadhihirisha kuwa, walipata umahiri mkubwa juu ya Chimbuko la Lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua mitazamo ya chimbuko la lugha ya Kiswahili kama ifuatavyo*:*

(a) *Chimbuko la Kiswahili ni Kameruni:Wataalamu waliochunguza kuhusu lugha za Kibantu wanadai kuwa chimbuko la Mame-Bantu ni Kameruni ambapo wameanza kuondoka katika eneo lao la asili huko Kameruni katika miaka 400K.K na kusambaa katika kingo za kaskazini za misitu ya Kongo na kuweka makazi yao kando ya mito ya Ukanda wa Afrika Mashariki mpaka ziwa victoria ambapo inasemekana kuwa walizungumza lugha ya Kiswahili*.

(b) *Wanaodai kuwa asili ya Kiswahili ni Kongo walifanya utafiti miaka 100 K.K ambapo wanadai kuwa Chimbuko la Mame-Bantu ni eneo la misitu ya Kongo. Wanadai kuwa*

*walikuwa Kongo na kutawanyika katika sehemu mbalimbali. Baadhi yao walikwenda Kusini mwa Afrika, wengine wakatawanyika kuelekea Kaskazini- Mashariki mwa Afrika ambao ndio wanaofikiriwa kuwa chimbuko la Wabantu katika upwa wa Pwani ya Afrika ya Mashariki ambao ndio wanaofikiriwa kuwa Waswahili waliozungumza lugha ya Kiswahili*. Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.



8. (a) chimbuko la Kiswahili ni Kameruni
Kameruni ni nchi iliyopo magharibi mwa bara
la Afrika ambapo karne nyingi zilizopita waliishi
wabantu waliojishughulisha na biashara ufugaji na
kilimo, Wataalamu wanadai kuwa palitokea
Janga la ukame na njaa kali iliyofanya wabantu
hao kutafuta maeneo ya makazi na nzuri kwa
kilimo. Hivyo walianza kuta wamenamba kufuata
msitu wa ikweta na kuingia Kongo na baadae
kuvuka mipaka na kuingia Afrika mashariki.

(b) Chimbuko la Kiswahili ni Kongo
Wataalamu wa nadharia hii wanadai kuwa Kiswahili
ni kikongo kwani hapo zamani miaka iliyopita
kana kulikuwepo na wabantu wanaoongea Kiswahili
hivyo kukatokea vita na njaa huko Kongo na
kusababisha wabantu hao kusambaa kote
Africa mashariki na kukutana na wabantu
wa eneo hilo, lugha iliyokuwa ikitumika ni

**Kielelezo Na. 8.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 8.


### 2.1.9 Swali la 9: Ufahamu

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutaja matumizi manne ya taaluma ya ufupisho katika shughuli za maisha ya kila siku. Asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango cha wastani kwani asilimia 41.2 ndio waliopata alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 9.




**Chati Na. 9:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 9.*


Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, asilimia 58.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0 hadi 1.5. Baadhi yao, hawakuelewa matakwa ya swali kwani walitaja umuhimu wa taaluma ya ufupisho badala ya matumizi ya taaluma hiyo katika shughuli za maisha ya kila siku. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja matumizi ya ufupisho kuwa ni; *unatoa mawazo maalum au makuu, huongeza maarifa, unasaidia kuongeza ujuzi wa kusoma na unasaidia kujua na kuongeza msamiati* badala ya kuelezea matumizi ya ufupisho kama vile; *hutumika wakati wa kutayarisha kumbukumbu au taarifa za mikutano, hutumika katika uandishi wa kumbukumbu za kila siku, hufupisha habari ndefu na kuokoa muda wa kusoma na hutumika sana katika uhariri na uandishi wa habari*. Vile vile, mtahiniwa mwingine aliandika majibu yasiyohusiana kabisa na taaluma ya ufupisho mfano; *huongeza ufahamu, humfanya mwanafunzi afikiri, humfanya mwanafunzi atumie stadi za kuandika za lugha*. Kielelezo Na. 9.1 ni majibu yasiyo sahihi yaliyotolewa na mmoja wa watahiniwa.




**Kielelezo Na.9.1:** Majibu yasiyo sahihi katika swali la 9.

Kielelezo Na. 9.1 ni majibu ya matahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali kwani alitaja vifaa vya mtaala badala ya matumizi manne ya taaluma ya ufupisho katika shughuli za maisha ya kila siku.

Aidha, asilimia 20.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 3 hadi 4 kwani waliweza kutaja hoja tatu hadi nne kwa usahihi. Hii inathibitisha kuwa, watahiniwa wa kundi hili walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ndogo ya *Ufupisho* na matakwa ya swali kwani waliweza kutaja matumizi ya taaluma ya ufupisho katika shughuli za maisha ya kila siku. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika matumizi ya ufupisho kuwa ni *hutumika katika uandishi wa kumbukumbu za kila siku, hufupisha habari ndefu na kuokoa muda wa kusoma, hutumika sana katika uhariri na uandishi wa habari na hutumika kuwasilisha mawazo ya mtu kwa ufupi katika mazungumzo.* Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


9. i) Ufupisho hutumika katika kuandaa hoja katika vikao mbalimbali
ii) Ufupisho hutumika katika kuandaa kumbukumbu za mikutano na vikao.
iii) Ufupisho hutumika katika kuandaa taarifa mbalimbali (ripoti)
iv) Ufupisho hutumika katika kuondoa hoja kwenye midahalo na mihadhara kama vile hotuba.


**Kielelezo Na. 9.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 9.

Katika kielelezo Na. 9.2, mtahiniwa alitaja matumizi sahihi ya taaluma ya ufupisho katika shughuli mbalimbali za maisha ya kila siku ingawa katika hoja ya (iv) alitoa mfano usio sahihi wa mihadhara kuwa ni hotuba .

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 20.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5 kwani walitaja hoja mbili sahihi badala ya nne tofauti na matakwa ya swali na wengine walitaja hoja mbili sahihi na nyingine hazikuwa sahihi. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *ufupisho unatumika kwenye masuala ya habari na utangazaji na ufupisho unatumika kuchukua dondoo kwenye mikutano au vikao vya maofisini*. Wengine walitoa hoja dhaifu hivyo kushindwa kueleweka kwa usahihi. Mfano mtahiniwa mmoja aliandika kuwa; *ufupisho hutumika vikaoni, habari za redioni na magazetini*.


### 2.1.10 Swali la 10: Upimaji

Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kutaja umuhimu wa mwalimu kutumia jedwali la upimaji kwa kutoa hoja nne. Swali lilijibiwa na watahiniwa wote (100%) waliofanya mtihani. Watahiniwa walipata ufaulu wa kiwango cha wastani kwani asilimia 62.4 walipata alama 2 hadi 4. Chati Na. 10 inafafanua viwango vya ufaulu vya watahiniwa.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 10.*

Asilimia 48.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 3 hadi 4. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya *jedwali la upimaji* na matakwa ya swali. Hivyo, waliweza kutaja umuhimu wa mwalimu kutumia jedwali la upimaji kwa kutaja hoja tatu hadi nne kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja hoja kama vile; *humsaidia mwalimu kupima mada zote zilizofundishwa kwa uzito unaotakiwa, kuangalia ni aina gani ya maswali anayoweza kuuliza kulingana na jazi la utambuzi, kuandaa mwongozo wa kujibia na kutunga idadi ya maswali kulingana na uzito wa kila mada*. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri na kupata alama za juu.




| | |
|---|---|
| 10 | i) Humsaidia Mwalimu Kuepuka kurudia rudia maswali |
| | ii) Humsaidia Mwalimu kujua Idadi ya maswali atakayotunga |
| | iii) Humsaidia Mwalimu kujua Mada atakazotungia Mtihani |
| | iii) Humsaidia Mwalimu kujua asilimia ya mtihani mzima. |

**Kielelezo Na. 10.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 10.

Kielelezo Na. 10.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutaja umuhimu wa mwalimu kutumia jedwali la upimaji kwa kutoa hoja nne kutokana na uelewa mkubwa alioukuwa nao kuhusiana na dhana ya jedwali la upimaji.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 262 sawa na asilimia 37.6 walipata alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa wa kundi hili, hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya dhana iliyotahiniwa pamoja na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja umuhimu wa upimaji kwa kuandika hoja kama vile; *humsaidia mwalimu kujua maendeleo ya mwanafunzi, kupata mrejesho wa alichofundisha, kujitathmini na kuandaa ripoti ya kila mwanafunzi* badala ya kutaja umuhimu wa mwalimu kutumia jedwali la upimaji kuwa ni; *humsaidia mwalimu kupanga maswali ya jaribio kulingana na ngazi au viwango vya ufahamu, kutunga maswali kulinga na malengo ya kila mada, kuonesha uwiano kati ya kilichofundishwa na kilichopimwa* na *kujua mgawanyo wa alama kwa kila swali*. Aidha, hoja kama; *humsaidia mwalimu kujua tabia za wanafunzi na kujua uelewa wa wanafunzi* zilitolewa na watahiniwa wengi. Kielelezo 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuelewa matakwa ya swali.


10 Umuhimu wa jedwali la Upimaji
(a) Kuweza kumsaidia kujua kama malengo mahususi yametimia
(b) humsaidia mwalimu kujua ni kwa kiasi gani wanafunzi wameelewa somo
(c) humsaidia mwalimu kujitathmini na kujua ni jinsi gani anaweza kuongeza maarifa na ya katika mchakato wa kujifunza na kufundisha
(d) humsaidia mwalimu kupima zana na mbinu anazotumia kama zinasaidiana na wanafunzi.

**Kielelezo 10.2:** Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 10.

Kielelezo Na. 10.2 ni majibu ya mtahiniwa ambayo ni kinyume na matakwa ya swali kwani alitoa hoja nne zinazoelezea umuhimu wa mwalimu kutumia andalio la somo badala ya jedwali la upimaji.

Hata hivyo, asilimia 14.0 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 2 hadi 2.5. Miongoni mwa sababu za watahiniwa hao kupata alama za wastani ni pamoja na kutaja hoja mbili kwa usahihi badala ya nne, kurudia hoja kwa maelezo tofauti na kutaja hoja


mbili sahihi na nyingine zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kuwa; *jedwali la upimaji linamsaidia mwalimu kuamua idadi ya maswali katika kila mada na kujua msawazisho wa maswali katika mada alizofundisha*. Kimsingi, maelezo haya yana maana ileile lakini yamewasilishwa kama hoja mbili tofauti. Vilevile, watahiniwa wengine walitaja hoja mbili zinazoelezea umuhimu wa jedwali la upimaji na nyingine mbili zinazoelezea umuhimu wa mwalimu kutumia jedwali la upimaji hivyo kupata alama za wastani.

## 2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha (Taaluma)

Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu (3) yaliyohitaji majibu marefu (insha) ambayo yalitungwa kutoka katika mada za *Taaluma ya Kiswahili*. Mtahiniwa alipaswa kujibu maswali mawili (2). Kila swali lilikuwa na uzito wa alama kumi na tano (15) hivyo, kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama thelathini (30). Aidha, kufaulu kwa watahiniwa kumegawanyika katika makundi matatu ambapo, mtahiniwa alipata kiwango hafifu cha kufaulu endapo alipata alama 0 hadi 5.5, wastani endapo alipata alama 6 hadi 10 na alihesabika kuwa na kiwango kizuri cha kufaulu iwapo alipata alama 10.5 hadi 15.

### 2.2.1 Swali la 11: Fasihi

Katika swali hili, mtahiniwa alipaswa kufafanua huku akieleza ubora na udhaifu wa kuhifadhi na kukusanya kazi za fasihi kwa kutumia njia zifuatazo: (a) *Mahojiano,* (b) *Maandishi* (c) *Kinasa sauti au tepu rekoda* (d) *Filamu na video na* (e) *Uchunguzaji*. Watahiniwa 682 sawa na asilimia 97.8 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kati yao, watahiniwa 597 sawa na asilimia 87.5 walipata alama 6 hadi 10.5 hivyo, kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kama inavyoonekana katika chati Na. 11.




**Chati Na. 11:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 11*.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, watahiniwa 411 sawa na asilimia 60.0 walijibu swali hili na kupata alama 6 hadi 10. Baadhi yao, walishindwa kutoa maelezo yanayojitosheleza katika kufafanua njia za kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi ingawa waliweza kueleza ubora na udhaifu katika kila njia. Vile vile, wapo walioweza kufafanua njia hizo kikamilifu huku wakishindwa kueleza ubora na udhaifu wa kila njia na wengine walifanikiwa kufafanua njia mbili hadi tatu badala ya tano hivyo, kupata alama za wastani.

Vile vile, asilimia 27.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 10.5 hadi 15. Watahiniwa wa kundi hili waliweza kufafanua njia nne hadi tano za kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi huku wakieleza ubora na udhaifu kwa kila njia. Aidha, walielewa matakwa ya swali pamoja na mada ndogo ya *Kuhifadhi na Kukusanya Kazi za Fasihi*. Kwa ujumla, waliweza kufafanua njia, kueleza udhaifu na ubora wa kila njia kama zilivyotolewa katika swali. Kielelezo Na. 11.1 ni sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa.

11. Fasihi ni sanaa inayotumia lugha ya maandishi au masimulizi ya mdomo ili kufikisha ujumbe kwa jamii fulani iliyokusudiwa. Fasihi imegawanyika katika aina mbili yaani fasihi andishi na fasihi simulizi ambazo zote hukusanywa na kuhifadhiwa kwa njia mbalimbali zifuatazo ni njia za kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi kwa kubainisha ubora na udhaifu wa kila njia.

Mahojiano ni njia inayotumika kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi ambapo ni mazungumzo kwa njia ya kuhojiana baina ya watu wawili. Ubora wa mahojiano ni kwamba mahojiano huambatana na vitendo mfano kuimba, kucheka n.k lakini udhaifu wake ni kwamba baadhi ya taarifa huweza kusahulika kwani uhifadhiwa kwa njia ya kichwa hivyo ni rahisi kupotea kumbukumbu.

Maandishi ni njia inayotumika pia katika kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi ambapo kazi mbalimbali kama vile nyimbo, hadithi, huweza kuandikwa katika maandishi mfano Riwaya n.k. Ubora wa mbinu/njia hii ni kwamba huhifadhiwa kwa muda mrefu lakini udhaifu wake ni kwamba hutumiwa na watu wanaojua kusoma na kuandika tu. hivyo ni mali ya muandishi tu.

Kinasa sauti au tepurekoda ni njia inayotumika kunasa na kurekodi sauti ya fanani au hadhira. Huhifadhi kazi za fasihi kwa njia ya sauti tu. Huhifadhiwa kwa muda mrefu lakini udhaifu wake ni kwamba fanani na hadhira hawawezi kuonana ana kwa ana.

Filamu au video, ni njia inayotumika kukusanya na kuhifadhi kazi ya fasihi ambayo sauti na picha huchukuliwa kwa njia ya video. Ubora wake ni kwamba sauti, picha na vitendo vya fanani huonekana lakini udhaifu wake ni kwamba hadhira hapati na nafasi ya kuuliza swali hivyo haipokei mabadiliko ya papo kwa papo.

Uchunguzaji ni kitendo cha kuchunguza mambo mbalimbali ya kifasihi kwa kutumia macho, maigizo n.k. Ubora wa mbinu au njia hii ni kwamba fanani na hadhira hukutana ana kwa ana lakini udhaifu wake ni kwamba taarifa zingine muhimu zinaweza zisipatikane kwani wakati mwingine fanani na hadhira hawawezi kukutana ana kwa ana.


Mwisho, kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi ni jambo muhimu sana kwani husaidia kurithisha amali za jamii, tamaduni, historia na kumbukumbu za matukio kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa lengo la kubundi-

**Kielelezo Na.11.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 11.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 85 sawa na asilimia 12.5 waliojibu swali hili walipata alama 0 hadi 5.5. Watahiniwa wa kundi hili, hawakuwa na uelewa wa kutosha

juu mada ndogo ya *Kuhifadhi na Kukusanya Kazi za Fasihi*. Walitoa hoja dhaifu zinazofafanua ubora na udhaifu wa njia husika zinazotumika kuhifadhi na kukusanya kazi za fasihi na wengine kutokufafanua kabisa njia hizo kinyume na matakwa ya swali. Wengine walishindwa kabisa kufafanua njia zote na kutoa udhaifu na ubora kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuwa *njia ya mahojiano husaidia kupata taarifa za papo kwa hapo* ilihali taarifa zinazotolewa si za papo kwa hapo bali hufanyika mahojiano baina ya watu wawili ambapo mmoja hueleza jambo la kifasihi kwa kina kama lilivyofanyika miaka iliyopita na taarifa hizo kuhifadhiwa. Aidha, alielezea kuwa ubora wa njia hii ni kutokuwa na gharama wakati mtafuta taarifa anaweza kutakiwa kusafiri mbali iwapo taarifa husika zitapatikana huko na kumfanya agharamike. Vilevile, hakufafanua njia ya maandishi na udhaifu aliotoa haukuwa sahihi kwani alieleza kuwa; *njia hii ina gharama* wakati mtafiti hujisomea vitini, vitabu na majarida mbalimbali yaliyokwishakuandaliwa badala ya kufafanua kuwa *njia hii haitoshi kumpatia mtafiti taarifa zaidi juu ya vipengele vya fasihi simulizi kama vile sauti, kiimbo, muziki, vitendo na uwasilishwaji wa jukwaani*.

Njia ya video au filamu haikufafanuliwa isipokuwa ubora na udhaifu ulifafanuliwa. Aidha, ufafanuzi wa ubora wa njia hiyo haukuwa sahihi kwani mtahiniwa aliandika kuwa; *hutunza kumbukumbu kwa muda mrefu* badala ya *vyombo hivi kwa kiasi kikubwa huhifadhi uhalisia wa mazingira ya fasihi simulizi na hutoa nafasi ya kuona uhalisia wa fasihi simulizi kama vile sauti, muziki* na *vitendo*. Katika kufafanua njia ya kinasa sauti au tepurekoda, mtahiniwa hakuweza kufafanua njia hiyo bali alielezea udhaifu wake na kushindwa kuelezea ubora wake. Aliandika kuwa; *hutunza kumbukumbu* badala ya *kumsaidia mtafiti kuhifadhi sauti ya mtambaji au mhojiwa na kupata sifa ambazo hazipatikani kwa njia ya maandishi, mfano kiimbo*. Aidha, njia ya uchunguzaji haikufafanuliwa ila ubora wake ulielezwa kwamba; *hukusanya data kwa kuona na kuhifadhi akilini au kuandika hivyo ni rahisi kutunza kumbukumbu* badala ya kueleza kuwa; *mtafiti anachunguza au kuangalia katika jamii ambamo anafanyia utafiti wake ambapo mtafiti anaweza akashiriki moja kwa moja au akarekodi matukio fulani na ni rahisi matokeo ya utafiti kuwa halisi iwapo mtafiti atakuwepo katika matukio*. Kielelezo Na.11.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.



11. Fasihi ni kazi ya Sanaa inayotumia lugha ya mazungumzo ili kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa kwa kutumia ubunifu. Uhakiki ni ubora na udhaifu wa kutumia njia za kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi.

(a) Mahojiano, ubora wa njia hii inasaidia kupata data na taarifa za papo kwa hapo, pia njia hii haina gharama. Lakini udhaifu wake ni kwamba kukosa wakati wengine uwezo wa kufanya mahojiano na kutumbukamba ni ya muda mfupi.

(b) Maandishi ubora wa njia hii inasaidia kutunza kumbukumbu ya muda mrefu na inasaidia kwa matumizi ya kizazi kijacho cha baadae. ~~Lakini~~ udhaifu wake ni kwamba njia hii ina gharama, mawahusu watu wanaojua kusoma na kuandika tu. Pia udhaifu mwingine njia hii haibadiliki ikishaandika imeandikwa mpaka lolee kipya.

c) Kinasa Sauti au tepurekoda. njia hii ni bora kwa sababu inatunza kumbukumbu lakini ina udhaifu wake watu wengine kipato cha chini wakishindwa kupata kazi hizo kwa sababu njia hii ina gharama.

d) Filamu au Video, ubora wa njia hii ni kwamba inatunza kumbukumbu na inaruhusu umakini wa watazamaji au hadhira. Lakini udhaifu wake ni ~~kwa~~ kwamba njia hii ina gharama hivyo basi inawafikia hadhira chache.

(e) Uchunguzaji, ubora wa njia hii ni kwamba ukusanya data kwa kuona na kuhifadhi akilini au kwa kuandika kwa hiyo ni rahisi kutunza kumbukumbu kwa muda mfupi lakini udhaifu wake unaweza kusahau baadhi ya vitu na kupoteza kumbukumbu.


Hivyo basi njia za kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi iwe ni andishi au simulizi ina ubora na udhaifu wake kwa hiyo ni lazima uwe makini unapochagua njia za kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi kwa ujumla.

**Kielelezo Na. 11.2 :** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 11.

Kielelezo Na. 11.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyefanikiwa kueleza udhaifu wa njia ya kinasa sauti na tepurekoda na kushindwa kueleza njia nyingine. Vile vile, alishindwa kueleza ubora wa njia zote kwa usahihi.

### 2.2.2 Swali la 12: Maendeleo ya Kiswahili

Swali lilimtaka mtahiniwa aeleze sababu sita zilizosababisha Kiswahili kisienee kwa urahisi nchini Uganda na Kenya. Asilimia 93.1 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Aidha, swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwa sababu asilimia 86.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 6 hadi 15. Chati Na. 12 inafafanua viwango vya ufaulu.




**Chati Na. 12:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 12.*

Baadhi ya watahiniwa waliopata alama za wastani ambazo ni kuanzia 6 hadi 10 walikuwa ni asilimia 71.0. Watahiniwa hao, walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi, wengine walishindwa kutoa utangulizi na hitimisho kwa usahihi na wengine hawakuandika kabisa. Aidha, wapo walioshindwa kuelezea sababu za Kiswahili kutokuenea kwa urahisi nchini Kenya na Uganda kwa kina na wengine kutoa hoja pungufu hivyo, kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea hoja nne ambazo ni; *kuwepo kwa vikundi vya makabila shupavu sehemu za kati ya nchi kama Wamasai na Wakamba ambao walizuia misafara ya biashara na wamisionari kutoka Pwani kwenda Bara, Kuwepo kwa wanyama wakali kama Simba na chui katika msitu wa Tsavo kuliongeza ugumu wa kuenea kwa Kiswahili, lugha za kienyeji kama Kikamba na Kikuyu zilitumika katika shughili za utawala mijini na vijijini, lugha za kienyeji ndio zilitumika kama lugha za kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi nchini Uganda na Kenya* na kuhitimisha kwa kuandika: *zilizopo hapo juu ni sababu za kuzuia Kiswahili kisienee kwa urahisi Uganda na Kenya*.

Vile vile, asilimia 13.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0 hadi 5.5. Wengi wao, hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* hususan mada ndogo ya *Kukua na Kuenea kwa Kiswahili*. Hivyo, waliandika sababu mbili sahihi na kuchanganya na sababu nyingine nne ambazo hazikuwa sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo alieleza sababu kama vile; *kutosanifiwa kwa lugha ya Kiswahili nchini Kenya na Uganda*, *kutokuwepo kwa misafara mingi ya utumwa wakati wa ukoloni*, *kuwepo kwa milima mirefu* na *upungufu wa watu waliokuwa wanaongea lahaja ambayo ingepelekea kusambaa kwa Kiswahili* badala ya kueleza sababu zilizosababisha Kiswahili kisienee kwa urahisi nchini Uganda na Kenya ambazo ni; *kuwepo kwa vikundi vya makabila shupavu sehemu za kati ya nchi kama Wamasai na Wakamba ambao walizuia misafara ya biashara na wamisionari kutoka Pwani kwenda Bara*, *Kuwepo kwa wanyama wakali kama Simba na chui katika msitu wa Tsavo kuliongeza ugumu wa kuenea kwa Kiswahili*, *lugha za kienyeji kama Kikamba na Kikuyu zilitumika katika shughili za utawala mijini na vijijini*, *lugha za kienyeji ndio zilitumika kama lugha za kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi nchini Uganda na Kenya*, *Kiswahili kilihusushwa na dini ya kiislamu kutokana na idadi kubwa ya wafanyabiashara walikuwa waislamu na Kiutawala nchini Uganda kulikuwa na tawala za kikabila ambazo zilitukuza na kuheshimu sana mila na lugha zao hivyo kuenzi lugha zao kuliko Kiswahili*.

Kwa ujumla, sababu zilizotolewa na mtahiniwa huyu hazikuwa na mashiko kwa sababu hazikudhihirika nchini Kenya na Uganda pekee bali hata nchini Tanzania ambamo lugha ya Kiswahili ilienea. Kwa mfano, nchini Tanzania kwa wakati huo hapakuwa na wataalamu wa lugha ya Kiswahili, kulikuwa na milima mirefu kama Kilimanjaro na Kiswahili kilikuwa bado hakijasanifishwa ila lugha hiyo ilienea kwa urahisi. Vile vile, mtahiniwa mwingine aliandika hoja nyingine kama vile; *upungufu wa vitabu au majarida mbalimbali* na *suala la uhaba wa wataalamu wa lugha ya Kiswahili*. Kielelezo Na. 12.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.

12. Kiswahili wakati wa ukoloni kilitumika katika shughuli mbalimbali kuhakikisha kinaenezwa na kukua lakini japo kilitumika Afrika ya mashariki, hakikuweza kutumika ipasavyo kenya na uganda kama kilivyoenea kwa wahisi nchini Tanzania Zifuatazo ndio sababu

Uteuzi wa baraza la kiswahili nchini. Huu ni uteuzi uliofanywa na kamati ya ya wanakiswahili, iliyohusisha wakati wa Afrika ya mashariki ilinyofanyikia Tanzania ambapo walikuja na malengo mbalimbali hivyo kupelekea kukua kwa kiswahili miaka ya 1940-1950.

Biashara ya utumwa Waarabu walipopita katika pwani ya Afrika ya mashariki walifanya biashara ya utumwa na kuwakuta watu wa tanganyika wakizungumza kiswahili na hivyo kusababisha kuenea. Sehemu walizotumia kuendesha biashara hizo ni sehemu kama bagamoyo, kilwa na pwani ya mombasa

Suala la manamba: Hawa walitumika na mkoloni kufanya shughuli mbalimbali ikiwemo shambani, kuvuna pamoja na kulima mkonge hivyo walikuwa wakizungumza kiswahili hivyo kusababisha kuenea kuliko kenya na uganda

Vyombo vya habari: Jambo lingine muhimu lililochangia kukua na kuenea kwa lugha ya kiswahili Tanganyika kuliko kenya na uganda ni vyombo vya habari kama vile magazeti, redio na televisheni mfano gazeti la sauti ya umma lililokuwa linahamasisha juu ya uhuru redio ya taifa pamoja na televisheni ya taifa

Elimu: Kupitia elimu nchini Tanganyika wakati wa ukoloni lugha ya kiswahili ilitumika pia katika kufundishia masomo mbalimbali hivyo kusababisha kukua nchini kuliko kenya na uganda.

Suala la dini: Wakoloni walitumia lugha ya kiswahili kufundisha dini kwa watu wa tanganyika tofauti na Kenya ilikuwa ikitumika lugha ya kingereza na kijaluo, kikuyu na kikikuyu jambo hilo lilifanya kiswahili kienee zaidi Tanganyika kuliko Kenya na Uganda.

Kiujumla suala la kuenea kwa kiswahili nchini kenya na uganda kulikuwa na kasi kama nchini Tanganyika hasa wakati wa ukoloni imesababishwa na shughuli mbalimbali kama zilivyoelezewa kwa afisaha hapo juu.

**Kielelezo Na. 12.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 12.

Katika kielelezo Na. 12.1, mtahiniwa alielezea sababu za kuenea kwa lugha ya Kiswahili maeneo mbalimbali ikiwemo nchini Tanzania badala ya kuelezea sababu zilizosababisha Kiswahili kisienee kwa urahisi nchini Uganda na Kenya.

Kwa upande mwingine, asilimia 15.9 ya watahiniwa walipata alama 10.5 hadi 15. Watahiniwa wa kundi hili, walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* hususan mada ndogo ya *Kukua na Kuenea kwa Kiswahili*. Hivyo, waliweza kuelezea sababu tano hadi sita zilizosababisha Kiswahili kisienee kwa urahisi nchini Kenya na Uganda. Aidha, walielezea hoja zao kwa mtiririko unaoleta mantiki, kuandika sehemu ya utangulizi na hitimisho linaloendana na swali na kutoa mifano ili kushadidia hoja hizo. Majibu yaliyotolewa na watahiniwa hao ni kama vile; *kuwepo kwa makabila shupavu sehemu za kati ya nchi kama wamasai na wakamba, lugha za kienyeji kama kikamba na kikuyu zilitumika katika shughuli za utawala mijini na vijijini, na kupelekea kutokuona haja ya kutumia lugha nyingine Kiswahili kikiwemo* na *matumizi ya lugha za kienyeji katika kufundishia shule za msingi*. Kielelezo Na. 12.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

12 Kuenea kwa Kiswahili ni hali ya kuongeze-
ka kwa watumiaji wa Kiswahili katika
eneo husika, wakati ukoloni ni hali ya
nchi moja kutawala nchi nyingine katika nyanja
za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Zifuata-
zo ni sababu za kutokuenea kwa wa-
nisi Kiswahili nchini Kenya na Uganda
wakati wa ukoloni:-

Kutumia lugha ya kiingereza katika
utawala, hivyo lugha ya kiingereza ilitumika
katika nyanja zote za kiuchumi na kisi-
asa na hivyo kukinyima fursa Kiswahili.

Imani potofu, Kenya na Uganda waliamini
kuwa Kiswahili kimeletwa na waarabu hivyo
mtu anayetumia Kiswahili atakuwa ni muumini
wa dini ya Kiislamu na hivyo wali-
kibeza Kiswahili.

Kuwepo kwa wanyama wakali katika
mbuga za Tsavo huko Kenya, kwa sababu
hiyo watu walishindwa kusafiri toka sehe-
mu moja na kwenda sehemu nyingine hivyo
ni ~~kut~~ lugha kuenea kwa kuingiliana kwa
watu.

Kutotumika Kiswahili katika elimu,
Kenya na Uganda walitumia lugha za
makabila katika ufundishaji na ujifu-
nzaji, hivyo Kiswahili hakikupata nafa-
si katika elimu na hivyo kushindwa
kuenea.

Kutumia lugha za makabila katika
shughuli mbalimbali za kijamii, mfano
biashara, siasa wakenya na waganda
walitumia lugha za makabila na hivyo
kukinyima fursa Kiswahili kuenea.

Kukibeza Kiswahili na kuona ni lugha
ya kikoloni, mfano waliamini kuwa lugha
ya Kiswahili imeletwa na wakoloni hivyo
hawakukubali kukitumia na kusababisha
kutokuenea kwa Kiswahili katika maeneo yao.


Hivyo basi, Kiswahili kilieneza kuenea
Tanzania kwa kutumika sana katika vyombo
vya habari, siasa elimu na biashara pa-
moja na usanifishaji.

**Kielelezo Na. 12.2 :** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 12.

### 2.2.3 Swali la 13: Matamshi na Lafudhi

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuchambua sifa sita za konsonanti za lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia mahali pa matamshi na kutoa mifano miwili ya konsonanti kwa kila sifa. Swali lilijibiwa na asilimia 8.8 ya watahiniwa waliofanya mtihani. Kiwango cha kufaulu

katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo asilimia 47.5 ya watahiniwa walipata alama 6 hadi 10. Chati Na. 13 inafafanua viwango vya ufaulu.




**Chati Na. 13:** *Ufaulu kwa Watahiniwa katika Swali la 13*.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, asilimia 52.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0 hadi 5.5. Miongoni mwao, hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya *Matamshi na Lafudhi* na matakwa ya swali hivyo, walichanganya sifa za konsonanti za Kiswahili kwa kuzingatia mahali pa matamshi na namna ya matamshi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja na kuelezea sifa za konsonanti kwa kuzingatia namna ya matamshi ambapo alitoa hoja kama vile; *vimadende, nazali, viyeyusho, vitambaza na vikwamizo* badala ya kuelezea sifa za konsonanti kwa kuzingatia mahali pa matamshi ambazo ni; *(i)* ***sifa ya midomo*** *ambapo huusisha mdomo wa chini na wa juu wakati wa matamshi yake. Mkondo hewa huzuiliwa na kuachiwa kwa kutumia mdomo wa chini na wa juu. Mfano; /m/, /b/ na /p/. (ii)* ***sifa ya midomo meno*** *huusisha vitamkwa ambavyo hutamkwa kwa mdomo wa chini kugusana na meno ya juu ambapo hewa hutolewa kwa kukwamizwa. Mfano; /v/, /f/. (iii)* ***sifa ya ulimi meno*** *hapa ncha ya ulimi husohea na kugusa meno ya mbele huku mkondo hewa ukiachiwa kwa kukwamizwa. Mfano; sauti 'dh' na 'th'. (iv)* ***sifa ya ufizi*** *inahusisha utamkaji wa vitamkwa ambapo ulimi hugusa kwenye ufizi nyuma kidogo ya meno ya mbele juu. Kwa mfano; /t/, /d/, /s/, /z/, /n/, /l/, na /r/. (v)* ***sifa za kaakaa gumu*** *hii inahusisha konsonanti ambazo wakati zinztamkwa ulimi hugusa kaakaa gumu../ (vi)* ***sifa ya kaakaa laini*** *hii inahusu konsonanti ambazo hutamkwa wakati ulimi unaposogea kugusa kaakaa laini na kubana mkondo wa hewa kisha kuachia kwa mlipuko. Kwa mfano, sauti 'g', 'k', 'gh', na 'ng`'. (vii)* ***sifa ya koromeo*** *konsonanti hii hutamkwa kwenye koromeo. Mfano, /h/*. Hata hivyo, watahiniwa wengine walielezea sifa mbili kwa usahihi bila kuweka mifano na wengine waliishia

kutaja sifa mbili hadi nne bila kutoa maelezo na kusababisha kupata alama hafifu. Kielelezo Na. 13.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.

13. Konsonanti za lugha ya kiswahili, ni maneno/(herufi) ambayo yapo katika mpangilio wa alfabeti na zikiungana na irabu hupelekea kuunda vitu mbalimbali mfano silabi huweza kuundwa. Zifuatazo ni sifa za konsonanti

Konsonanti haziwezi kusimama peke yake na kuleta maana, hivyo konsonanti zikiungana na irabu tunapata nomino au majina ya watu, vitu na mahali mfano <u>B</u>a<u>b</u>a Bb ni konsonanti zilizopelekea kuunda nomino Baba pia <u>Ma</u><u>m</u>a tuna pata nomino ambayo imetokana na muunganiko wa konsonanti na irabu.

Konsonanti huonyesha matendo ya watu na kupelekea kukamilisha sentensi, mfano <u>k</u>u<u>l</u>a K L hizi ni konsonanti pia katika neno I<u>mb</u>a M b hizi ni konsonanti kwahiyo konsonanti hutambulisha matendo mbalimbali ya watu.

Konsonanti zinaunda sentensi, kupitia hoja hii tunaona sentensi nyingi za kiswahili zimeundwa na konsonanti peke ambapo konsonanti ikiungana na irabu au konsonanti ikiungana na konsonanti nyingine pamoja na silabi mfano Cheza <u>Ch</u> konsonanti pamoja na silabi <u>z</u>a z ni konsonanti

Konsonanti huonesha mpangilio wa alfabeti, kutokana na hoja hii tunaona jinsi ambavyo konsonanti zina mpangilio maalum wa alfabeti katika lugha ya kiswahili mfano b c d g h k l m n ... z pia katika mpangilio huo husaidia kupanda na kushuka kwa sauti ya lugha ya kiswahili katika utamkaji wa maneno.

Konsonanti zina sifa ya kuunda maneno mbalimbali ya kiswahili, kupitia hoja hii konsonanti zitaunda neno endapo zitaungana na irabu mbili na konsonanti mbili au zaidi mfano mtu ana potamka neno "feedha" hapa tunaona jinsi konsonanti inavyosifiwa katika kuunda neno feedha <u>f</u> ni konsonanti na <u>dh</u> ni konsonanti <u>e</u> a ni irabu

Konsonanti zinakamilisha tungo mbalimbali za kiswahili, kutokana na hoja hii ni kwamba konsonanti zitaunda silabi na silabi zitaunda neno na kuunda sentensi hivyo sentensi zitaunda tungo mbali mbali za kiswahili mfano <u>M</u>wenda ana akili sana konsonanti ni <u>M</u> w <u>n</u> d <u>n</u> K L s n hizi ni konsonanti.


Kwahiyo kutokana na konsonanti za kiswahili hupelekea watu kutambua umuhimu wa konsonanti pamoja na kuondoa utata katika kutamka maneno ya kiswahili.

**Kielelezo Na. 13.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 13.

Katika kielelezo Na. 13.1, mtahiniwa alieleza sifa za konsonanti za Kiswahili zisizohusiana na dhana ya matamshi na kusababisha majibu yake kuwa kinyume na matakwa ya swali.

Uchambuzi zaidi wa takwimu unaonesha kuwa, asilimia 14.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 6 hadi 10. Hii imethibitisha kuwa, watahiniwa wa kundi hili walielewa matakwa ya swali na mada iliyotahiniwa kwa kiwango cha wastani. Walichanganya baadhi ya dhana wakati wa kutoa ufafanuzi na mifano ya sauti katika sifa husika. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kuwa; *sifa ya meno ni pale ambapo midomo ya chini inakutana na meno ya juu na kutoa sauti mbalimbali mfano /m/ na /p/* badala *ya mdomo wa chini hukutana na meno ya juu ambapo wakati wa utamkaji wake, hewa huzuiliwa na kutoa sauti /f/ na /v/.* Mtahiniwa huyo, alichanganya mifano ya sauti za meno (/f/ na /v/) na za midomo (/m/ na /p/ ingawa maelezo yake yalikuwa sahihi. Changamoto nyingine zilizowafanya watahiniwa wapate ufaulu wa wastani katika swali hili ni pamoja na; kutokufafanua sifa kwa kina, kutoa maelezo yasiyohusiana na sifa husika mfano kuelezea sifa ya midomo katika sifa ya meno na kutokutoa mifano katika kila sifa kama yalivyokuwa matakwa ya swali.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 32.8 walipata alama 10.5 hadi 15 kwa sababu walielewa matakwa ya swali pamoja na mada ya *Matamshi na Lafudhi* hususan katika kipengele cha sauti za konsonanti. Mtahiniwa mmojawapo alielezea sifa za konsonanti kwa kuzingatia mahali pa matamshi na kuweka mifano. Mtahiniwa huyo, alielezea sifa hizo kuwa ni; *sifa ya ufizi ambapo ncha ya ulimi hukutana ufizi na kuzalisha sauti /t/, /d/, /s/, /z/ na /l/, sifa ya koromeo ambapo konsonanti hutamkiwa kwenye koromeo mfano /h/, sifa ya kaakaa gumu ambayo inahusisha konsonanti ambazo wakati zinatamkwa ulimi hugusa kaakaa gumu mfano, sauti 'ch', 'j', na 'sh', sifa ya midomo meno ambapo vitamkwa hutamkwa kwa mdomo wa chini kugusana na meno ya juu mfano, sauti 'f' na 'v'* na *Sifa ya kaakaa laini ambapo konsonanti hutamkwa wakati ulimi unapogusana na kaakaa laini mfano, sauti 'g' 'k', gh' na 'ng''*. Kielelezo Na. 13.2 ni sehemu ya sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.



13\. Konsonanti ni sauti zinazotamkwa kwa mkwamo wa hewa kutoka katika mapafu. Mfano wa konsonanti ni /s/, /b/, /t/, /g/, /m/ na nyinginezo pia kuna konsonanti vikwamizi mfano /z/ na /s/. Zifuatazo ni sifa za konsonanti kuzingatia mahali pa matamshi:

Hutamkwa kwa meno na ncha ya ulimi: Baadhi ya konsonanti huwa na sifa ya kutamkwa katika meno ya juu na ya chini na ncha ya ulimi. Mfano /ð/, /th/, /dh/.

Hutamkwa kwa midomo miwili: Kuna baadhi ya konsonanti hutamkwa pale zinapokutana midomo miwili. Mfano /p/ na /b/, hapo ndio konsonanti hizo huzaliwa.

Hutamkwa katika kaakaa gumu na mzizi wa ulimi: Pia hii ni sifa ya baadhi ya konsonanti, ambapo kaakaa gumu hugusana na mzizi wa ulimi ili kuzalisha konsonanti. Mfano /k/, na /g/.

Hutamkwa kwa meno ya juu na mdomo wa chini: Meno ya juu yanapokutana na mdomo wa chini huzaa baadhi ya konsonanti. Mfano /v/ na /f/.

Hutamkwa kwa ncha ya ulimi na meno ya juu: Baadhi ya konsonanti huwa na sifa ya kutamkwa pale inapogusana ncha ya ulimi na meno ya juu. Mfano


**Kielelezo Na. 13.2 :** Sampuli ya Sehemu ya majibu sahihi katika swali la 13.

## 2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha (Utaalamu)

Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu (3) yaliyohitaji majibu marefu (insha) ambayo yalitungwa kutoka katika mada za *Utaalamu wa Kufundisha Kiswahili*. Mtahiniwa alipaswa kujibu maswali mawili (2). Kila swali lilikuwa na uzito wa alama kumi na tano (15) hivyo, kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama thelathini (30). Aidha, kufaulu kwa watahiniwa kumegawanyika katika makundi matatu ambapo mtahiniwa alikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu endapo alipata alama 0 hadi 5.5, kiwango cha wastani endapo alipata alama 6 hadi 10 na kiwango kizuri iwapo alipata alama 10.5 hadi 15.


### 2.3.1 Swali la 14: Upimaji

Swali lilimtaka mtahiniwa kuelezea ngazi sita za upimaji kwa nyanja ya utambuzi, kisha atunge swali kwa kila ngazi kwa kutumia mada ndogo ya "Aina za Tungo" kwa kidato cha tatu. Swali lilijibiwa na asilimia 35.6 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwa sababu asilimia 81.0 ya watahiniwa walipata alama 6 hadi 15. Chati Na. 14 inafafanua viwango vya ufaulu vya watahiniwa.




**Chati Na. 14:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 14.*

Asilimia 41.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 10.5 hadi 15. Huu ni uthibitisho kuwa watahiniwa hao walielewa vizuri matakwa ya swali pamoja na Nyanja mbalimbali za Upimaji. Waliweza kufafanua ngazi tano hadi sita na kutunga swali kwa kila ngazi, katika nyanja ya utambuzi kwa kutumia mada ndogo ya ‘Aina za Tungo’ kwa kidato cha tatu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea ngazi hizo kuwa ni; *maarifa, hii ni nyanja inayopima uwezo wa mwanafunzi kukumbuka mambo mbalimbali au maarifa aliyojifunza,* mfano wa swali ni *‘taja aina nne za tungo’* na *ufahamu: kupitia nyanja ya ufahamu, mwanafunzi hupimwa uelewa au jinsi anavyoelewa mambo aliyojifunza darasani, mfano wa swali ni ‘eleza maana ya kishazi’*. Aidha, mtahiniwa huyo aliweza kuelezea ngazi nyingine kwa usahihi kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 14.1.



14. Nyanja za upimaji ni hatua ambazo hutumika kupima malengo mahususi katika ufundishaji na ujifunzaji. Kupitia ngazi ya utambuzi kuna nyaja sita ambazo hutumika kupima wanafunzi, Nyanja hizo ni kama zifuatazo na aina ya swali ambalo linaweza kuulizwa katika mada Ndogo ya "Aina za Tungo" kwa kidato cha tatu.

Maarifa; Hii ni nyanja inayopima uwezo wa mwanafunzi kukumbuka mambo mbalimbali au maarifa aliyojifunza. Hapa vitenzi kama taja, bainisha, Toa hutumika. Mfano wa swali linaloweza kuulizwa ni "Taja aina nne za tungo."

Ufahamu; Kupitia nyanja ya ufahamu, Mwanafunzi hupimwa uelewa au jinsi anavyoelewa Mambo aliyojifunza darasani. Vitenzi kama, eleza, Fafanua hutumika. Mfano, "Eleza maana ya kishazi huru"

Matumizi ni nyanja nyingine katika ngazi ya utambuzi. Hapa mwanafunzi hupimwa uwezo wako wa kutumia mambo mbali aliyofundishwa katika mazingira halisi. Mfano. "Tumia kishazi huru kutunga sentensi tano"

Uchambuzi. Hapa mwanafunzi hupimwa uwezo wa kufafanua mambo mbalimbali kwa kubainisha mfanano, tofauti, umuhimu au hasara. Mfano wa swali linaloweza kuulizwa katika nyanja hii ni "Fafanua aina mbalimbali za sentensi"

Utungaji. Katika nyanja hii, kinachopimwa ni uwezo wa mwanafunzi kujumuisha au kuunganisha mambo mbalimbali aliyojifunza na kupata wazo kuu. Mfano wa swali linaloweza kutumika ni "Tunga sentensi tano zinazoonyesha tungo kirai"

Tathmini. Hii ni nyanja ya juu zaidi katika nyanja zote. Tathmini hupima kiwango cha juu cha utambuzi wa mwanafunzi katika kutathmini Maarifa aliyofundishwa kwa mfano swali la tathmini linaweza kuwa "Tathmini umuhimu wa kutumia tungo mbalimbali katika kuwasiliana"

Kwa kuhitimisha, nyanja au ngazi ya utambuzi ni muhimu katika suala la upimaji kwa mfano hutumika katika kuandaa maswali ya mtihani, pia humsaidia mwalimu kupangilia ufundishaji au mada zake kutoka kiwango cha chini cha utambuzi kwenda cha juu.

**Kielelezo Na. 14.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 14.


Kielelezo Na. 14.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuelezea ngazi sita za upimaji kwa nyanja ya utambuzi ingawa katika ngazi ya tano, alikosea jina na mfano wa swali ambapo aliandika utungaji badala ya uundaji na maelezo yake hayakujitosheleza.

Vile vile, asilimia 39.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 6 hadi 10 kutokana na kushindwa kufafanua hoja kwa kina. Pia, wengi wao walishindwa kutumia vitenzi sahihi kwenye maswali waliyotunga katika ngazi husika pamoja na kushindwa kuandika utangulizi na hitimisho zuri linalohusiana na kilichoulizwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *eleza aina mbili za fasihi* kama mfano wa swali katika ngazi

ya maarifa (kukumbuka). Kimsingi kitenzi eleza kinapima uelewa wa mwanafunzi kuhusu jambo fulani hivyo, hakipaswi kutumika kwenye ngazi ya maarifa kwa sababu ngazi hiyo hupima kumbukumbu na vitenzi vyake ni kama vile; orodhesha, taja, ainisha na toa.

Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa (19.0%) walipata alama 0 hadi 5.5. Miongoni mwao, walishindwa kuelewa matakwa ya swali na hivyo kutoa majibu amabayo ni tofauti na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika zana za upimaji kama vile; *maswali na majibu, mazoezi, majaribio, majadiliano, mitihani na uchunguzi* badala ya kuelezea ngazi sita za upimaji kwa nyanja ya utambuzi ambazo ni; *Maarifa (kumbukumbu) ni uwezo wa kukumbuka mambo mbalimbali yaliyofundishwa*. *Mfano: Taja aina tatu za tungo katika lugha ya Kiswahili*. *Ufahamu ni uwezo wa kueleza jambo kwa maneno mengine Mfano: Eleza kwa kifupi dhana ya tungo*. *Matumizi ni uwezo wa kutumia maarifa aliyoyapata mwanafunzi katika mazingira mbalimbali*. *Mfano: tunga sentensi sahili kwa kutumia kitenzi kishirikishi "ni"*. *Uchambuzi ni uwezo wa kutenganisha, kuonesha uhusiano na kufasili mambo yanayoibuka kutokana na uchambuzi husika. Mfano: Chambua aina za maneno zinazounda sentensi ifuatayo 'Mtoto mdogo amelala vizuri'. Uundaji ni uwezo wa kuweka habari kwa kifupi, kulinganisha mawazo na kuyaweka katika hali ya umoja au kuweka vitu pamoja ili viweze kuibuka na muundo mpya kabisa. Mfano: Unda vishazi tegemezi vinne kwa kutumia kiambishi cha o-rejeshi* na *Tathmini ni uwezo wa kupima uzuri au ubaya, ubora au udhaifu wa jambo fulani. Mfano, Si kila tungo ni sentensi. Jadili kauli hiyo kwa mifano dhahiri.*

Aidha, watahiniwa wengine walidhihirisha uwezo mdogo juu ya mada ya *Upimaji* hususan kipengele cha jedwali la upimaji. Watahiniwa hao, walishindwa kufuata mpangilio sahihi wa ngazi katika nyanja ya utambuzi kwa mfano kuanza kuelezea ngazi ya tathmini badala ya maarifa au kumbukumbu. Vile vile, mtahiniwa mwingine alielezea aina za maswali kwa mfano, maswali ya *kuoanisha, kujaza sehemu iliyowazi, maswali ya kweli au si kweli na maswali ya insha* na mwingine alielezea aina za upimaji ambazo ni; *upimaji wa awali, upimaji gunduzi, upimaji endelevu na upimaji tamati*. Wengine walielezea ngazi moja hadi mbili kwa usahihi bila kuweka mifano hivyo, kupata alama hafifu. Kielelezo Na. 14.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kulingana na matakwa ya swali.



14. Upimaji ; Ni tendo la kuchambua
a mbinu mbalimbali zilizo tumika kwa lengo
la kutaka kuboresha katika ufundishaji na
ujifunzaji: Hivyo basi upimaji unaweza kuwa
mgawanyo ni, upimaji wa awali, upimaji endel
elevu, upimaji tathmini na upimaji tamati; Hivyo
basi upimaji huo nyanja sita za upimaji kwa
ngazi ya utambuzi ni kama ni:-
Kumsaidia mwalimu kutambua uw
ezo wa mwanafunzi wake; Hivyo mwalimu
huweza kumpima mwanafunzi kwa kumu
uliza swali ili aweze kutambua uwezo wake
kwa mfano swali anaweza mwambia mwanafunzi
tafa eleza maana ya tungo. mwanafunzi akijibu
bu tayari mwalimu anatambua uwezo wake.
Kumsaidia mwalimu kuboresha -
mbinu ya ufundishaji na ujifunzaji; Hivyo basi
mwalimu huweza kutumia upimaji ili ku
weza kubaini mbinu alotumia ni sahihi
kwa watoto mfano mbinu ya maswali na
majibu. swali taja aina za tungo. mwana
funzi anataja.
Kumsaidia mwalimu kuhamia -
ngazi nyingine ya mafunzo; katika nyanja
hii mwalimu hutumia mada hii ya aina
za tungo ili kuweza kubaini kama alicho
fundisha kimeeleweka kwa mfano ana
uliza swali kuna aina ngapi za tungo
mwanafunzi akajibu bila utata na
wote kwa ufasaha wa kujibu ndipo
tungo mwalimu ana kila haja budi
kuhamia ngazi nyingine ya mafunzo.
Kumsaidia mwalimu kupanga
nafasi katika ushindani; katika nyanja
hii mwalimu hupanga nafasi katika ushi
ndani baada ya kuta pata kile alichokiuliza
ana kuuliza kwa mwanafunzi kwa
mfano swali Ainisha aina za tungo. kila
mwanafunzi kaweza kuainisha hivyo atakae
za kuangalia aliyeainisha vizuri zaidi.
Kumsaidia katika utoaji wa-
vyeti; pia nyanja ya upimaji humsaidi
a mwalimu katika ugawaji wa vyeti mfa
no cheti cha taaluma atampatia mtu
ambae anaonekana alifanya vizuri
katika kile alichokiuliza. swali-
eleza na fafanua aina za tungo kwa
mfano. Hivyo husaidia.
Kumsaidia mwalimu kubaini maen
deleo ya mwanafunzi wake; katika nyanja
hii mwalimu hubaini maendeleo ya mwana
funzi wake kwa kutumia maswali
mfano eleza maana ya tungo mwana
funzi atakaejibu ana pata kutambua
tatizo na kuanza kuifanyia usahihisha
ji au ufuatiliaji wa kazi zake.
Hivyo basi ninyema mwalimu
kutumia nyanja ya upimaji ili kuwe
za kusahihisha matatizo ya mwana-
funzi wao na kuweza kuweka uhusiano
wa karibu baina ya mwalimu na
mzazi wa mwanafunzi au mwalimu
na mwanafunzi ili kuweza kusahihisha

**Kielelezo Na. 14.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 14.

Katika Kielelezo Na. 14.2, mtahiniwa alielezea umuhimu wa upimaji badala ya ngazi sita za upimaji kwa nyanja ya utambuzi na kutunga swali moja kwa kila ngazi kwa kutumia mada ndogo ya "Aina ya Tungo" kwa kidato cha tatu.

### 2.3.2 Swali la 15: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia

Katika swali hili mtahiniwa alipaswa kuelezea changamoto sita atakazo kutana nazo mwalimu, anapotumia mbinu ya ziara mafunzo kufundisha kipera cha matambiko katika fasihi ya Kiswahili. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, watahiniwa 455 sawa na asilimia 65.3 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Aidha, swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwani asilimia 85.7 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama 6 hadi 10 kama inavyofafanuliwa kwenye chati Na.15.




**Chati Na. 15:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 15*.

Asilimia 61.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 6 hadi 10. Watahiniwa hao, walishindwa kufafanua baadhi ya hoja walizotoa na wengine waliweza kuelezea changamoto tatu hadi nne badala ya sita. Pia, wengine waliachanganya hoja sahihi na zisizo sahihi, walitaja hoja sahihi na kushindwa kutoa maelezo ya kina na wengine kushindwa kuandika utangulizi mzuri na hitimisho au kutokuandika kabisa.

Vile vile, asilimia 24.6 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama 10.5 hadi 15. Hii inaonesha kwamba, watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia*. Waliweza kuelezea changamoto tano hadi sita atakazokutana nazo mwalimu anapotumia mbinu ya ziara ya mafunzo katika kufundisha

kipera cha matambiko katika fasihi ya Kiswahili kama vile; *mwalimu asipotoa maelekezo ya kutosha kuhusu malengo ya ziara hiyo na msingi wa mada ya matambiko, wanafunzi wanaweza kudhani ni safari ya mapumziko na burudani*, *baadhi ya wanafunzi wanaweza kuingiwa na hofu kwa sababu matendo ya matambiko kadhaa yanatisha* na *ugumu wa kutambua mhusika atakaye waelekeza kama ana weledi na tajiriba ya kutosha katika matambiko*. Kielelezo Na. 15.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.

15. Ziara ya Mafunzo ni mbinu ya kujifunza ambapo mwalimu na wanafunzi huondoka na kwenda kujifunza nje ya eneo la shule kama vile kwenye maeneo ya kihistoria, kwenye jamii na kwingineko. Lakini katika njia hii mwalimu huweza kukutana na changamoto mbalimbali mfano kama akifundisha kuhusu kipera cha tambiko kwa jamii fulani kama ifuatavyo. "Matambiko" ni mila ya jamii au imani ya jamii fulani, Matambiko yanaweza kufanywa kwenye maeneo makaburi na kwingineko. Ifuatayo ni changamoto anazoweza kukumbana nazo mwalimu wakati akitumia ziara ya kujifunza kwa kipera cha Matambiko.

Walimu hukumbwa na changamoto kwa baadhi ya jamii ambazo zinakuwa hazipo tayari kuonesha mila ya jamii yao; pindi mwalimu anapohitaji kufanya ziara ili wanafunzi waweze kujifunza kipera cha Matambiko kutoka katika jamii zetu.

Kuwepo kwa baadhi ya wanafunzi ambao hawako tayari kujihusisha na mambo ya mila na desturi; Mfano kuna wanafunzi ambao wao Jamii zao hazitambui mambo ya mila na desturi hivyo kumpa mwalimu changamoto pindi anapohitaji kufanya ziara pindi anapofundisha kipera cha matambiko.

Sehemu za matambiko zinakuwa ni za siri sana, Mfano kwenye misitu ya kutisha, mawe makaburi, milima, hivyo kumpa mwalimu changamoto ya kufanya ziara ya mafunzo kupitia kipera cha Matambiko ambapo baadhi ya sehemu hizo zinakuwa na usalama mdogo.

Kuwepo kwa sheria kali sehemu ambazo Matambiko hufanyika, Mfano kuna vitu ambavyo havipaswi kushikwa na kila mtu, hivyo kuna baadhi ya wanafunzi huweza kuvigusa bila idhini ya muongozaji. hivyo kufanya walimu kupata changamoto pindi anapotumia mbinu ya ziara kufundisha kipera cha Matambiko.


Gharama ni changamoto kwa walimu wanapotumia mbinu ya ziara ya Mafunzo kufundisha kipera cha Matambiko, Mfano kwa shule za mjini wanakumbwa na changamoto pindi wanapotaka kujifunza mambo ambayo yanapatikana kwenye mila na desturi, kwa sababu mila nyingi zipo maeneo ya vijijini..

Matambiko hufanywa kwa muda na kwa shida maalumu ambapo hufanywa na wazee pamoja na wahusika wa jamii, hivyo kupelekea changamoto kwa walimu pindi wanapotumia mbinu ya ziara ya Mafunzo kujifunza kipera cha Matambiko na kupelekea ugumu kwa jamii kufanya Matambiko kwa sababu wanaamini yanafanywa kwa shida maalumu zinazoikumba jamii.

Hata hivyo Mbinu ya ziara ya masomo kujifunza kipera cha Matambiko kinaweza kisilete changamoto kwa walimu kama watawasiliana na jamii husika kwamba wanahitaji kufanya ziara ili walimu wapewe muda gani wanaweza kufanya ziara ili kujifunza kipera cha Matambiko kwa ufanisi.

**Kielelezo Na. 15.1 :** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 15.

Hata hivyo, watahiniwa wachache sawa na asilimia 14.3 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama 0 hadi 5.5. Miongoni mwao, walishindwa kuelewa matakwa ya swali hivyo, wakaandika madhara ya kutokutumia mbinu ya ziara ya mafunzo badala ya changamoto atakazokutana nazo mwalimu atakapotumia mbinu ya ziara ya mafunzo kufundisha kipera cha matambiko katika fasihi ya Kiswahili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kuwa; *wanafunzi kutokuelewa kwa uhalisia*, *wanafunzi kushindwa kuwa wabunifu, kupata ujumbe usio sahihi kutokana na kutokuelezewa kitu na mhusika moja kwa moja, kutokufurahia somo* na *kushindwa kuelewa matambiko mbalimbali kwa kina* badala ya kuelezea changamoto atakazokutana nazo mwalimu kama vile; *baadhi ya wanafunzi huenda wakashindwa kuhudhuria mafunzo hayo kwa kukosa fedha za kugharamia ziara, mwalimu asipotoa maelekezo mapema juu ya msingi wa safari hiyo wanafunzi wanaweza kudhani ziara hiyo ni sehemu ya mapumziko hivyo malengo yanaweza yasifikiwe, baadhi ya wanafunzi wanaweza kuingiwa na hofu kusikiliza na kushuhudia masimulizi na matendo ya matambiko, siyo kila jamii ina kawaida ya kuweka wazi, utaalamu wa mambo ya mila unahitaji tajiriba na uelewa wa kutosha katika mambo hayo hivyo kuna ugumu wa kupata wataalamu wenye weledi, kuna uwezekano baadhi ya wanafunzi wakashindwa kuhudhuria kutokana na imani za kidini.* Vile vile watahiniwa wengine waliandika majibu ya kubuni ambayo hayakuhusiana na matakwa ya swali kutokana na uelewa mdogo juu ya dhana iliyotahiniwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja kama vile; *kutokuwa na maandalizi ya zana, kutokujiamini kutumia njia ya ziara, kutokuwepo kwa vyombo vya usafiri na kuingia katika ugomvi na jamii inayozunguka*.



15.

Ziara: Ni mbinu inayotumika katika njia ya ufundishaji na ujifunzaji napo humshirikisha mwalimu na mwanafunzi katika kujifunza. Nathibitisha kauli hii kwamba si kweli walimu hukutana na changamoto wanapotumia mbinu ya ziara ya mafunzo kufundisha kipera cha malambiko katika fasihi ya kiswahili kwa kutumia hoja zifuatazo?

Huwahusisha ufundishaji na ujifunzaji: Hii katika mbinu hii inamsaidia mwalimu na mwanafunzi katika ufundishaji na ufundishaji kwani huweza kujifunza zaidi kwa kutumia uhalisia wa mada yenyewe.

Pia Ujenga kumbukumbu ya kudumu: Katika ujifunzaji na ufundishaji njia ya ziara huweza kumjengea mwanafunzi na mwalimu ~~ny~~ kumbukumbu ya kudumu.

Humsaidia mwanafunzi kujifunza mambo mengi: Katika kutumia mbinu ya ziara katika ufundishaji na ujifunzaji humfanya mwanafunzi kujifunza mambo mengi hivyo huweza kuelewa somo kwa urahisi.


Humsaidia mwanafunzi kuwa mdadisi: Katika njia ya ziara inamsaidia mwanafunzi kuwa mdadisi wa mambo ambayo atakayoyaona hivyo humjengea ~~tu~~ uelewa mkubwa wa kufikiri pale anapofanya ziara ya somo husika.

**Kielelezo Na. 15.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 15.

Katika kielelezo Na.15.2, mtahiniwa alielezea umuhimu wa ziara ya mafunzo badala ya changamoto atakazokutana nazo mwalimu atakapotumia mbinu hiyo katika kufundisha kipera cha matambiko katika fasihi ya Kiswahili.


### 2.3.3 Swali la 16: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Kiswahili

Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua faida sita za kitabu cha kiada katika kufundisha na kujifunza somo la Kiswahili. Asilimia 98.3 ya watahiniwa 697 waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwa sababu asilimia 97.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 6 hadi 15. Chati Na. 16 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa.




**Chati Na. 16:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 16.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 56.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 10.5 hadi 15 kwa kuwa walikidhi matakwa ya swali na walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana na matumizi ya kitabu cha kiada. Watahiniwa hao, waliweza kufafanua faida sita za kitabu cha kiada katika kufundisha na kujifunza somo la Kiswahili kama vile; *hubeba maudhui yanayoendana na kiwango cha elimu cha mwanafunzi, utoshelevu wa maudhui na mazoezi, kimesheheni vielelezo, picha na michoro ya kutosha inayomwezesha mwanafunzi kuelewa somo vizuri, kinakuwa na lugha inayolingana na walengwa na humsaidia mwanafunzi kupata maarifa zaidi*. Kielelezo Na. 16 ni sampuli ya majibu sahihi katika swali hili.



16 Kitabu cha kiada ni miongoni mwa vifaa vya ntaala ambacho hutumiwa na mwalimu pamoja na mwanafunzi pia. Kitabu hiki huonesha mpangilio wa mada zote ambazo mwalimu anatakiwa kuzifundisha kwa mada husika.

Zifuatazo ni faida za kutumia kitabu cha kiada katika ufundishaji na ujifunzaji.

Humsaidia mwalimu kufundisha mada kwa mpangilio maalum. Kitabu cha kiada humsaidia mwalimu kuchagua maada atakazoanza nazo yaani nyepesi kwenda ngumu na ngumu kwenda rahisi.

Humsaidia mwanafunzi kuitumia pindi kujifunza pindi anaporudi nyumbani; kitabu cha kiada humsaidia mwanafunzi pale anaporudi nyumbani kujifunza au kurudia kile alichofundishwa darasani.

Humsaidia mwanafunzi kutumia picha na michoro ile kujenga dhana halisia ya mada anayojifunza. Kitabu cha kiada kinamfanya mwanafunzi kuongeza maarifa kupitia michoro na picha zilizomo ndani yake.

Huwasaidia wanafunzi ambao hawajahudhuria kipindi kujifunza kile kilichofundishwa darasani; kitabu cha kiada ni muhimu kwa mwanafunzi kwa kinamjenga mwanafunzi mwenyewe.

Humsaidia mwanafunzi kufanya mazoezi mbalimbali ili kuongeza uelewa kwa sehemu ya mada husika. Kitabu hiki ni muhimu sana kwa sababu humpa mwanafunzi hali ya utayari wa kufanya mazoezi mbalimbali.

Humjengea mwalimu hali ya kujiamini pindi anapofundisha; hii humsaidia pale mwalimu anapofundisha mada kutumia mawazo tofauti tofauti ya waandishi ambayo humuongezea maarifa zaidi na kufanya kutoa mifano iliyo hai kwa wanafunzi wake.

Hivyo basi kitabu cha kiada ni muhimu sana katika shughuli ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kinamsaidia mwalimu kuwa na maarifa mengi pamoja na kufundisha mada kwa mpangilio maalum bila kuacha ata kipengele ata kimoja

**Kielelezo Na. 16.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 16.

Vile vile, watahiniwa 279 sawa na asilimia 40.7 walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa hao, waliweza kufafanua faida tatu hadi nne za kitabu cha kiada kwa usahihi na wengine walishindwa kutoa maelezo yanayojitosheleza katika hoja walizotoa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuwa: *kitabu cha kiada ni kifaa*

*anachotumia mwalimu kama silaha akishindwa kujibu hoja darasani anasoma kwenye kitabu hivyo mwalimu hana budi kutembea nacho popote na anapaswa kuingia nacho darasani kwakuwa ndiyo silaha yake.* Aidha, wapo walioshindwa kutoa utangulizi na hitimisho kwa usahihi hivyo, kukosa alama za sehemu hizo. Mfano mtahiniwa mmoja wapo aliandika utangulizi kuwa; *kitabu cha kiada ni mchakato wa kufundishia na kujifunzia unaomsaidia mwalimu na mwanafunzi kusoma mara kwa mara.*

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa wachache sana (2.3%) walipata alama 2.5 hadi 5.5 kwani hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya dhana ya kitabu cha kiada. Wengi wao, walielewa matakwa ya swali lakini walishindwa kujenga na kutetea hoja zao kikamilifu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua faida za kitabu cha kiada kuwa ni; *humsaidia mwalimu kwenda na wakati kwa sababu ya maendeleo ya sayansi na teknolojia*, *huwafanya wanafunzi kufurahia somo, kusoma kwa bidii na huendana na sera za elimu za nchi za nje*. Pia, watahiniwa wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na kushindwa kutoa utangulizi mzuri na hitimisho. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika utangulizi kuwa; *kitabu cha kiada ni kitabu ambacho kimeidhinishwa na taasisi ya elimu na wizara ya elimu kufundishia na kujifunzia*. Kielelezo Na. 16.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

16. Ufundishaji na Ujifunzaji ni mbinu au mchakato anaoutumia mwalimu kufikisha maarifa kwa mwanafunzi; Kitabu cha kiada ni mwongozo anaoutumia mwalimu katika kufundisha muhtasari moja kwa moja. Faida za kutumia kitabu cha kiada katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la kiswahili ni kama:

Husaidia kujua mada mbali mbali za kiswahili; hii ni faida ya kutumia kitabu cha kiada katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la kiswahili humsaidia kujua mada mbalimbali za kiswahili katika. Kitabu cha kiada ni kitabu cha muhtasari kwa kuwa kinaandaliwa na mada za muhtasari moja kwa moja.

Kupata maarifa; hii ni faida za kutumia kitabu cha kiada katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la kiswahili, hii humsaidia mwalimu kupata maarifa kutumia kitabu cha kiada hii inaandaliwa na muhtasari moja kwa moja katika kupata maarifa.

Husaidia kujua miundo mbalimbali za kiswahili. ni faida za kutumia kitabu cha kiada katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la kiswahili.

Husaidia kujua malengo na maudhui ya jamii; Faida za kutumia kitabu cha kiada katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la kiswahili hii huwezesha kujua malengo na maudhui ya jamii katika kutumia fasihi yake. Kutumia kitabu cha kiada katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la kiswahili.

Husaidia kujua zana au vifaa za kutumia katika kazi mbalimbali za kiswahili, hii ni faida za kutumia kitabu cha kiada katika kujifunza na kufundisha kwa kujua somo la kiswahili husaidia kujua zana.

Husaidia kujua vipindi mbalimbali vya kiswahili; hii ni faida ya kutumia kitabu cha kiada katika ufundishaji na ujifunzaji katika somo la kiswahili husaidia kujua vipindi mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la kiswahili.

Kwahiyo basi, ufundishaji na ujifunzaji ni mbinu za mchakato anaoutumia malimu ili kufikisha maarifa kwa mwanafunzi. Kama husaidia kujua maada mbalimbali za kiswahili, kupata maarifa, kujua miundo mbalimbali za kiswahili kujua male

**Kielelezo Na. 16.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 16.

Kielelezo Na. 16.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyefafanua faida nne za mwalimu kutumia muhtasari wa somo la Kiswahili badala ya kitabu cha kiada. Aidha, aliweza kutaja hoja sahihi ya *kupata maarifa* na *kumwezesha mwalimu kuandaa zana ingawa maelezo yake hayakujitosheleza* hivyo, kupata alama za chini.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU CHA WATAHINIWA KWA MADA

Mtihani wa 721 Kiswahili ulikuwa na maswali (16) yaliyotoka katika mada 11. Uchambuzi wa kufaulu kwa watahiniwa katika mada hizo unaonesha kuwa, watahiniwa wamefanya vizuri katika mada 6 ambazo ni sawa na asilimia 54.5 ya mada zote zilizotahiniwa. Mada hizo ni; *Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili (97.7%), Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili (94.7%), Zana za Kufundishia na Kujifunzia (90.8%), Fasihi (87.6%), Maendeleo ya Kiswahili (77.9%)* na *Upimaji (71.8%).*

Watahiniwa walipata kiwango kizuri cha ufaulu katika mada hizo kwa sababu walionesha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada na matakwa ya kila swali. Vile vile, waliweza kujieleza vizuri kwa lugha inayoeleweka, kujenga hoja katika mtiririko unaoleta mantiki pamoja na kufuata taratibu na kanuni za uandishi hasa katika maswali ya insha.

Pia, watahiniwa walipata kiwango cha wastani cha ufaulu katika mada 4 ambazo ni sawa na asilimia 36.4 ya mada zilizotahiniwa. Mada hizo ni ; *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia (61.7%), Matamshi na Lafudhi (54.7%), Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili (47.1%)* na *Ufahamu (41.2%)*. Sababu za watahiniwa kupata ufaulu wa wastani katika mada hizo ni pamoja na uelewa wa wastani wa mada zilizotahiniwa, kutokuandika idadi ya hoja kulingana na matakwa ya swali na kutokufuata kanuni za uandishi hususan katika maswali ya insha.

Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu kilikuwa hafifu katika mada ya *Uhakiki wa kazi za Fasihi (37.3%)*.Watahiniwa walipata kiwango hafifu cha kufaulu katika mada hiyo kutokana na uelewa mdogo wa mada, kutokuelewa matakwa ya swali pamoja na kutokujibu swali kikamilifu. Mchanganuo wa ufaulu wa watahiniwa kwa mada umefafanuliwa katika kiambatisho.

## 4.0 HITIMISHO

Ripoti hii inaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika mtihani wa 721 Kiswahili kwa mwaka 2020 kilikuwa kizuri kwani asilimia 99.28 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walipata alama 40 na zaidi. Aidha, kiwango hicho kimetokana na watahiniwa kuwa na umahiri wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa na kuelewa matakwa ya maswali mbalimbali. Kiwango hiki cha ufaulu kimeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2019 ambapo wastani wa kiwango cha kufaulu kilikuwa ni asilimia 99.07.

Hata hivyo, uchambuzi wa kina ulifanyika na kubaini uwepo wa changamoto mbalimbali zilizowafanya baadhi ya watahiniwa kushindwa kufanya vizuri. Changamoto hizo ni uelewa mdogo wa matakwa ya swali, mada zilizotahiniwa kama vile mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*, uelewa mdogo wa jinsi ya kujibu maswali pamoja na kutokuwa na umahiri wa kujieleza kwa ufasaha hususan katika kujenga hoja zenye mtiririko unaoleta mantiki. Aidha, changamoto nyingine zilizobainika ni baadhi ya watahiniwa kushindwa kutoa mifano sahihi ya kushadidia hoja walizotoa.

Mwisho, Baraza linatarajia kuwa, taarifa hii ya uchambuzi kuhusu majibu ya watahiniwa itatia chachu kwa walimu tarajali na wakufunzi kuelewa makosa yanayosababisha watahiniwa wachache kutokujibu maswali vizuri. Aidha, itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu cha somo hili kutokana na kuelewa kasoro zinazofanywa na baadhi ya watahiniwa ambazo husababisha washindwe kujibu maswali vizuri.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Baraza la Mitihani la Tanzania linaona kuwa, kiwango cha ufaulu wa watahiniwa kimeongezeka kutokana na jitihada mbalimbali za wadau, maboresho ya miundo mbinu na mafunzo kazini kwa wakufunzi yanayofanywa na Serikali. Hata hivyo, ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu katika somo hili inashauriwa:

(a) Wizara inayohusika ione haja ya kuandaa warsha kwa wakufunzi ili waongeze ujuzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*, *Ufahamu* na *Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili*.

(b) Wakufunzi watumie rejea za ziada kama magazeti na majarida anuai kufundishia mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi* ambayo imeonekana kuwa na kiwango hafifu cha kufaulu.

(c) Wakufunzi watumie zaidi mazoezi ya mazungumzo, mkoba wa kazi na kazi mradi kama zana za upimaji hususan katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*.

(d) Wakufunzi wanahimizwa kuwapa walimu tarajali mazoezi ya mara kwa mara ya kuhakiki kazi mbalimbali za fasihi katika kipengele cha lugha hususani tamathali za semi.

(e) Wakufunzi wawasisitize walimu tarajali kusoma kwa makini na kutafsiri maswali ya mtihani kwa kina kabla ya kujibu.

**MUHTASARI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA SOMO LA KISWAHILI**

| Na | Mada | Namba ya Swali | Ufaulu Katika Kila Swali (%) | Wastani wa Ufaulu Katika Mada (%) | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili | 16 | 97.7 | 97.7 | Vizuri |
| 2. | Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili | 6 | 94.7 | 94.7 | Vizuri |
| 3. | Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili | 3 | 90.8 | 90.8 | Vizuri |
| 4. | Fasihi | 11 | 87.6 | 87.6 | Vizuri |
| 5. | Maendeleo ya Kiswahili | 8 | 68.9 | 77.9 | Vizuri |
| | | 12 | 86.9 | | |
| 6. | Upimaji | 10 | 62.5 | 71.8 | Vizuri |
| | | 14 | 81.0 | | |
| 7. | Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia | 5 | 69.9 | 61.7 | Wastani |
| | | 7 | 29.4 | | |
| | | 15 | 85.7 | | |
| 8. | Matamshi na lafudhi | 4 | 61.8 | 54.7 | Wastani |
| | | 13 | 47.5 | | |
| 9. | Vifaa vya Mtalaa wa Somo la Kiswahili | 1 | 47.0 | 47.0 | Wastani |
| 10. | Ufahamu | 9 | 41.2 | 41.2 | Wastani |
| 11. | Uhakiki wa Kazi za Fasihi | 2 | 37.3 | 37.3 | Hafifu |